# *Kusikia, Kutambua, Kutenda Kwa Neno La Mungu*

Sasa, hizi kanda, ile ya mkutano huu asubuhi ya leo, haiuzwi, ni kwa ajili ya Kanisa tu au kwa mtu fulani, kwa sababu ni juu ya Mafundisho. Na katika mikutano huko nje, husababisha machafuko, kwa sababu ni vigumu wawili wetu kuona macho kwa macho kikamilifu, lakini tunapaswa kuwa moyo kwa moyo, hata hivyo. Lakini hiyo, sisi katika maskani hapa, kanda hizi ziko, unaona juu ya . . . Ni kwa marafiki tu, na kadhalika.

2 Sasa hebu na tuviinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi tu kwa ajili ya maombi. Ni wangapi wangependa kukumbukwa wakati mmeinamisha vichwa vyenu? Kwa mkono ulioinuliwa tu, ukisema, "Bwana, mimi ni—mimi ni mhitaji leo, na ninahitaji neema Yako," hata iwe ni nini.

3 Baba yetu wa Mbinguni, sasa tunakaribia Kiti Chako cha rehema, kwa sababu tumeombwa kufanya hivi. Na tuliambiwa na Mwana Wako, na Mwokozi wetu, kwamba ikiwa tutakuomba Wewe chochote katika Jina Lake, tutapewa. Kwa hivyo, Bwana, tukijua kwamba tunaishi katika vivuli vya Kuja Kwake, na sasa tumesimama katika vivuli vya rehema Zake, basi tungeuliza, Bwana, kwamba utachagua, kwa Roho Mtakatifu, yale mambo ambayo tunapaswa kuomba. Nasi tunahisi asubuhi ya leo, kwamba haitakuwa kinyume na Neno Lako au haki Yako kuu, na rehema na neema Yako, kwamba ikiwa tutauliza kwamba tutatembelewa leo na Roho Mtakatifu. Ili aingie katikati yetu na apambanue mawazo ya mioyo yetu, kutufunulia mahali pa udhaifu wetu, na kuponya magonjwa yetu, na kufunga mioyo iliyovunjika, na kuokoa waliopotea, na kuandaa watu kwa ajili ya Kuja Kwake. Bwana, sikia maombi haya.

4 Sasa tutasoma Neno Lako. Na—na tunaomba, Bwana, kwamba kwenye somo letu la shule ya Jumapili asubuhi ya leo, kwamba Wewe utaleta muktadha wa usomaji na utaifunua kwa mioyo yetu. Kwa sababu, tunakuja hapa kwa kusudi moja. Kusudi hilo, peke yake, ni kukujua Wewe vizuri zaidi. Sisi tulio Wakristo, kwa Imani, tunataka kukujua zaidi. Wale ambao bado hawajawa Wakristo, wanataka kukujua Wewe kama Mwokozi wao. Wale ambao ni wagonjwa, wanataka kukujua Wewe kama Mponyaji wao. Nasi tunaomba ya kwamba kusiwepo na mtu atakayetoka kwenye jengo hili, mtupu, lakini ili kila haja itimizwe kikamilifu, na kila hamu kutimizwa, na kila—kila mtu awe na furaha, na waende kutoka kwenye jengo, wakisema,

kama wale wanaotoka Emau, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, wakati alipoongea nasi njiani?" Kwa maana tunaomba haya katika Jina la Yesu. Amina.

5 Sasa kwako wewe ambaye unataka kufungua kwenye Kitabu chako. Kwa kawaida, nimegundua, kwamba katika ibada za kiinjilisti, kwamba yapata dakika ishirini au thelathini tu huleta matokeo bora zaidi kwa kuingiza ujumbe wa kiroho, na kisha wito wa madhabahuni. Lakini hii ikiwa ni shule ya Jumapili, sitaki kuifanya hivyo asubuhi ya leo. Ninajisikia kuongozwa zaidi kuchukua muda wangu na kuzungumza juu ya Neno.

6 Sasa, ikiwa mtu yeyote hana starehe, anahisi baridi sana, jambo pekee unalopaswa kufanya ni . . . Ndugu yangu, msimamizi, yuko nyuma ya kanisa pale, inua tu mkono wako namna *hiyo* huko nyuma, kwake, naye atarekebisha hali ya joto. Na tunataka uwe starehe na ujisikie vizuri kabisa. Na usikilize Neno, kwani tunamtumainia Roho Mtakatifu kutufundisha Neno la Mungu. Na hivi nyote mnaweza kusikia vizuri, huko nyuma? Kama mnaweza, inueni mikono yenu, ikiwa mna— mnaweza kusikia vizuri. Hiyo ni nzuri.

7 Sasa nataka mfungue pamoja nami, nina mafungu kadhaa yaliyoandikwa hapa, na Maandiko. Kwa hivyo nataka mfungue pamoja nami, kwanza, kwenye Kitabu cha Warumi, Warumi, sura ya 9. Na tunataka kusoma kwa ajili ya somo la Maandiko, kwanza, katika Warumi 9:11.

> *(Kwa maana kabla hawajazaliwa wale watoto, wala hawajatenda neno jema wala baya, ili lisimame kusudi la Mungu la kuchagua, si kwa sababu ya matendo, bali kwa sababu ya nia yake aitaye;)*
>
> *aliambiwa hivi, Mkubwa atamtumikia mdogo.*
>
> *Kama ilivyoandikwa, Nimempenda Yakobo,* na *Esau nimemchukia.*

8 Mungu aongeze baraka Zake kwenye usomaji huu wa Maandiko. Na sasa kwa ajili ya fungu, kuunga mkono somo langu, nataka kuchukua hili kama fungu: *Kusikia, Kutambua, Kutenda Kwa Neno La Mungu*. Naomba nirudie hilo tena. "Kusikia, na kutambua, na kisha kutenda kwa Neno la Mungu."

9 Sasa, tunafahamu kabisa, sisi watu ambao tunachunguza Maandiko mchana na usiku, na kusoma magazeti yetu na kusikia watangazaji wa habari, kwamba ulimwengu huu sasa umesimama mkononi mwa nguvu mbili kuu za kiroho. Na zote ni nguvu za kidini. Na ninaamini kwamba nguvu hizi kuu hivi karibuni zitafikia kwenye kichwa. Na nguvu hizi mbili kuu zote ziliwakilishwa katika wana hawa wawili wa Isaka. Jinsi ambavyo Mungu, katika hekima Yake isiyo na kikomo, ametuonyesha mambo yote kimbele kwa njia ya mfano; ili kwa mambo haya tuweze kujua, kwa hakika, ni nini kilicho

mbele yetu. Ilifanywa iwe dhahiri sana, kwamba Mungu na Neno Lake, na maumbile na ulimwengu Wake, vimepangwa pamoja kikamilifu kabisa, kwamba hata mwe—mwenye dhambi anaweza kuona kwamba jambo fulani linakaribia kutendeka. Mungu ameipanga hivyo. Hakuna mtu asiye na udhuru.

10 Sasa, tunaona katika wana hawa wawili kwamba wakati wao, hata kabla hawajazaliwa, walikuwa vitani wao kwa wao. Ingawa mama yao bikira. . . Kwa maana, alikuwa bikira, Rebeka mrembo ambaye aliolewa na uzao wa haki wa ahadi ya Mungu, Isaka; kwamba walikuwa ni waaminio wawili wa Mungu waliowekwa wakfu, waliojazwa na Roho, walioteuliwa kimbele kwa ndoa yenyewe ambayo waliungana pamoja kwayo. Mungu aliijua kimbele. Na ni vipi kitu kama hicho kingeweza kupitia mama huyo mmoja, na baba mmoja? Mmoja, mtu mbaya sana; na mwingine, mtu mzuri sana; na jinsi ambavyo mtu mzuri alionekana kuwa mbaya, na yule mbaya alionekana kuwa ndiye mzuri.

11 Sasa hiyo ni, daima imekuwa, daima itakuwa mpango wa Mungu. Mungu hawezi kubadilisha mpango Wake. Kwa sababu, Yeye hufanya mpango Wake uwe mkamilifu, kwa sababu ni sehemu Yake.

12 Katika bustani ya Edeni, dhambi ilikuwa nzuri sana hata ilimvutia Hawa kutoka kwa haki, kwenda dhambini. Na katika bustani ile ile ambapo kulikuwa na mti wa Uzima, kulikuwa na mti wa mauti pia.

13 Tungeijua leo kama sheria ya kulinganisha. Kwamba, palipo na mema, kuna mabaya; palipo na haki, pana batili. Na hatutaweza kamwe, bila kujali mazingira yetu, kuwa na uwezo wa kujitikisa kutoka kwenye uwepo wa mojawapo. Kwa sababu, Paulo alisema, "Nitakapo kutenda mema, basi mabaya yapo." Mwenye dhambi hataweza kujitikisa atoke kwa Mkristo, Mkristo kutoka kwa mwenye dhambi. Kutakuwa na shahidi hapo wa haki, na ushuhuda wa batili, kila wakati. Na wewe unafanya chaguo lako. Inakubidi uchukue upande mmoja au ule mwingine.

14 Lakini katika wana hawa wawili, ni ajabu kujua kwamba, kabla hawajazaliwa, wote wawili uzao ule ule, kutoka kwa Isaka, ambao ulikuwa ni ahadi. Sasa, somo letu ni refu kidogo, na ninataka kupata msingi wa kutosha hata mweze kuona haswa kile ninachozungumzia. Na mwana wa kwanza, Esau, aliyezaliwa; tunaona kuwa sio tu walikuwa wakigombana na kupigana ndani ya tumbo la mama yao, lakini walitoka ndani yake, wakipigana, Esau akitoka nje, na Yakobo ameshika kisigino chake. Na wangali wanapigana.

15 Na jinsi hiyo, jinsi ingeweza kutoka kwa baba au mama aliye mkamilifu, safi, aliyechaguliwa, mtakatifu, aliyejiweka wakfu! Kwa hivyo kuiwekea msingi, kwamba, Mungu huita kwa

uteuzi. Lazima iwe. Haijalishi baba na mama yako walikuwa wazuri kiasi gani, jinsi walivyokuwa wazuri, baba na mama yako walikuwa Wakristo kiasi gani, bado inakutegemea kama mtu binafsi, msimamo wako mbele za Mungu. Somo hili linafundisha kwamba, kwamba wao, watoto wote wawili, kulikuwa na hata wateule na walioitwa na Mungu, baba na mama, mwanamke bikira na mwanamume mtakatifu, ambaye hatimaye alikuja kuwa hata kupitia uzao wake alikuja Yesu Kristo. Alizaliwa kama mmoja kutoka kwa wafu. Alijaribiwa, baba yake kabla yake. Naye aliahidiwa, kupitia uzao huu wa Isaka, kwamba ulimwengu wote utaokolewa. Na kutoka kwa mtu kama huyo, na damu yake safi kabisa hata Mungu hangemruhusu hata yule Mfilisti hata amguse huyo mama, baada ya Ibrahimu kumkabidhi kwake. Mungu aliitesa nyumba yake, akasema, "Wewe ni sawa na mtu aliyekufa," akishikilia mkondo huo wa damu safi. Na huyo Rebeka, mama mwenye haki, mtakatifu, aliyetumwa na Mungu na aliyeitwa na Mungu. Na kutokana na hiyo mbegu takatifu akatokea mwasi na mwaminio. Unaona? Kwa hivyo iko katika wito wa Mungu, uteuzi wa Mungu.

16 "Na kabla hata mmoja hajazaliwa, Mungu alisema, 'Ninampenda Yakobo na kumchukia Esau,' kabla ya kuzaliwa hata mmoja wao." Kwa hivyo tunapaswa kujisikiaje. Mtu ambaye Mungu anazungumza na wewe na kukualika uje kwenye meza Yake na Nyumbani Kwake, na kuwa mwana au binti Yake, hakuna kitu kikuu kama hicho.

17 Wavulana hawa wawili, ikiwa tutaangalia asili yao, mmoja wao alikuwa mtu wa kiroho, huyo alikuwa Yakobo. Na mtu wa kimwili alikuwa Esau. Lakini wote wawili walikuwa wa kidini. Na kitu hicho hicho kimefanyika kote katika wakati, wa kimwili na wa kiroho.

18 Esau alimwakilisha mtu wa dunia, wa kawaida, anayeegemea dini, lakini kamwe hawezi. Haikuwa ndani yake kuifanya. Asingeweza kuifanya. Hakuwa kamwe ndani yake kuweza kupanda kupita mambo ya ulimwengu, mambo ya kimwili.

19 Lakini, Yakobo, ilikuwa rahisi sana kwake kuifanya. Sasa, Yakobo, kusudi moja Yakobo alikuwa nalo, na hiyo ilikuwa kwamba alitamani haki hiyo ya mzaliwa wa kwanza, haijalishi aliipataje, bora tu aliipata.

20 Na roho hiyo ya kuzaliwa mara moja bado inawakilishwa ulimwenguni leo, na inakuja kwenye kichwa sasa: mwaminio wa kiroho; na mtu wa kimwili, mwaminio wa kimwili. Hakuna mtu angeweza kusema hawakuwa wote wawili wa kidini. Walikuwa. Hawakusema kwamba mmoja alitumikia "sanamu" na yule mwingine "Mungu." Wote wawili walikuwa watumishi wa Mungu.

21 Sasa, zingatia kwa makini Maandiko sasa juu ya mada hii, kwa sababu nina hakika itakusaidia. Unaona? Sasa, "Si kila mtu asemaye, 'Bwana, Bwana' ataingia, bali yule afanyaye mapenzi ya Baba Yangu aliye Mbinguni."

22 Sasa ukiangalia, Yakobo alikuwa na kitu kimoja ambacho alitaka, kwa sababu, kulingana na Neno, baraka na ki—kitu kizuri kiliwekwa katika haki ya mzaliwa wa kwanza. Na, Yakobo, hilo ndilo lilikuwa lengo lake pekee, jambo pekee alilokuwa nalo akilini mwake lilikuwa "pata haki hiyo ya mzaliwa wa kwanza." Naye Esau aliidharau. Yule ambaye hasa alikuwa nayo, aliidharau, au aliionea aibu. Lakini Yakobo aliitaka bila kujali anaipataje, aliitaka.

23 Ndivyo ilivyo kwa mwaminio wa kiroho leo hii. Hajali ni kiasi gani unamcheka, ni dhihaka kiasi gani unayofanya, ni dhihaka kiasi gani inambidi kutenda kwa akili ya kimwili. Kusudi lake pekee ni haki ya mzaliwa wa kwanza. Anataka kumfikia Mungu, sababu imezaliwa ndani yake. Hawezi kujiepusha.

24 *Yakobo* linamaanisha "mchukua mahali pa mwingine" au "mdanganyifu." Lakini baada ya kupata na kumiliki haki ya mzaliwa wa kwanza, alibadilishwa. Hilo ni badiliko, kimwili. Wakati huo aliitwa, Yakobo, "mtawala pamoja na Bwana," ambaye ameshindana naye mwereka.

25 Mwaminio wa kimwili leo hii, "Loo, mradi tu ninaenda kanisani na kufanya yaliyo mema, inaleta tofauti gani?" Hilo ni kundi la Esau. Angali anaifanyia mzaha na kuidharau haki ya mzaliwa wa kwanza, haijali. Lakini Yakobo aliipenda.

26 Naye mwanamume wa kiroho leo hii, na mwanamke wa kiroho, waliochaguliwa, waliokusudiwa kimbele na Mungu kuja kwenye Uzima wa Milele, ikiwa watalazimika kuuza kila kitu walicho nacho, ikiwa watalazimika kuondoa jina lao kwenye kila kitabu cha kanisa katika taifa, bado wanataka haki hiyo ya mzaliwa wa kwanza. Ndilo jambo la pekee ambalo ni muhimu kwao, "kupata tu haki hiyo ya mzaliwa wa kwanza," hiyo tu. Haijalishi jinsi gani, ni kiwango gani wanapaswa kufika, ikiwa watalazimika kushuka madhabahuni na kulia, boo-hoo, ikiwa watalazimika kukimbia kupitia ma—ma—maeneo hayo na kurudi nyuma na kurekebisha mambo, na kuuza walicho nacho, au—au kutoa kila kitu walicho nacho na kuwa msafiri na mgeni, haijalishi. Wanataka haki ya mzaliwa wa kwanza. Hiyo ndiyo tu wanayovutiwa nayo, haki ya mzaliwa wa kwanza. Sasa, usiwalaumu watu hao. Hawawezi kujizuia. Walikusudiwa kimbele kwa hilo, wakachaguliwa kwa hilo.

27 Na kisha tunaona kwamba hawa wawili, watu wa kimwili na wa kiroho, ndivyo ilivyotokea kila wakati. Ndivyo ilivyo leo hii. Imekuwa hivyo kila wakati.

28 Kaini na Habili. Katika bustani ya Edeni, wakati Edeni ilipoumbwa, kulikuwa na miti miwili ili mtu achukue chaguo lake. Moja, yeye kuwa wa hekima; huo mwingine, yeye akawa Uzima. Kulikuwa na wavulana wawili, Kaini na Habili, wote wawili wakiwa wa kidini. Mmoja wao alitamani Uzima wa Milele, naye akamtolea Mungu, kwa imani, dhabihu iliyo bora zaidi kuliko Kaini. Mfano kamili wa makanisa leo hii: kanisa la kawaida, kanisa la kiroho. Na hapana shaka ila kwamba ninazungumza na matabaka yote mawili sasa hivi, na labda kwa kanda nitazungumza na makumi ya maelfu yao.

29 Lakini, angalia, kanisa la kawaida, ni kanisa tu la kimwili. Hawawezi kamwe kupanda juu ya kitu hicho kidogo cha "Nilijiunga na kanisa. Ikiwa ninaenda kanisani, ikiwa nitafanya kadri niwezavyo, hayo ndiyo yote Mungu anayohitaji." Sasa, hilo ndilo jambo lile lile ambalo Kaini alifanya. Alienda akatengeneza madhabahu. Alitoa dhabihu, akaleta matunda ya nchi. Naye akasema, "Hii hapa, Mungu. Hiyo ndiyo iliyo bora zaidi niliyo nayo. Ichukue au uiache." Hivyo ndivyo mwaminio wa kimwili anavyoamini leo hii. "Bwana, nitaenda kanisani. Nitajiunga na kikundi bora zaidi ambacho ninaweza kupata. Nitatoa malipo yangu kwa kanisa. Nitafanya yaliyo sahihi. Sasa, hii hapa iliyo bora zaidi ninayoweza kufanya. Nitasaidia kununua makaa kwa ajili ya mjane. Au, nitawapa watoto mavazi." Hayo yote ni sawa, hakuna la kusema dhidi yake. "Lakini hayo ndiyo, ni hayo tu. Ukitaka, chukua; ikiwa hutaki, si lazima uichukue." Sasa, huo ndio mtazamo wa kanisa la kimwili leo hii.

30 Lakini kanisa la kiroho! Habili, kwa ufunuo, kwa neema, aliona zaidi ya hapo, na kwa imani alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora zaidi kuliko Kaini. Na ilishuhudia haki yake, Mungu.

31 Jambo hilo hilo lilifanyika kwa Ishmaeli na Isaka. Mmoja alikuwa wa kimwili, na mwingine alikuwa wa Roho. Mmoja, wa mjakazi; mmoja, wa mwanamke huru.

32 Ilitokea jambo lilo hilo katika Israeli na Moabu, makanisa mawili makubwa yakija pamoja. Na wakati Israeli walikuwa wanataka kwenda mahali pao palipoahidiwa, kanisa la kiroho, watu wa Yakobo, Israeli njiani; Watu wa Esau walikutana nao, Moabu, kanisa lenye nguvu. Na kiongozi mkuu wa kanisa, Balaamu, alishuka kumlaani ndugu yake, lakini alikuta kwamba hangeweza kumlaani ndugu yake. Alishindwa, na upofu wa macho yake, kuona mpango uliokusudiwa kimbele, huo, na kuona Neno la Mungu.

33 Kwanza, "Imani huja kwa kusikia, kusikia Neno la Mungu." Ndipo mwaminio analisikia, analitambua, na kuliweka katika matendo. Mtu wa kimwili atalisikia, sauti Yake, lakini kamwe. . .*Kusikia* maana yake ni "kuelewa" Hilo. Angalia, ni kuangalia kitu; lakini *kukiona*, ni "kukielewa". "Mtu

asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuona au kuelewa Ufalme wa Mungu."

34 Sasa, hii hapa Israeli inakuja, wakija na ahadi ya Mungu, kwamba walikuwa wakielekea nchi ya ahadi. Sio makafiri, lakini waaminio, waaminio wa Mungu yule yule ambaye Israeli ilikuwa naye, walitoka kujaribu kumlaani ndugu yake, kwa sababu alisema ndugu yake ni, hakika hakuwa mwadilifu kwa sababu alikuwa amefanya mambo mengi ambayo yalikuwa mabaya. Lakini, unaona, alishindwa kuona uteuzi.

35 Jambo lilo hilo na Esau na Yakobo! Esau alionekana kuwa mtu bora. Alitulia na kufanya mambo ya hisani. A—alimtunza baba yake mzee kipofu, akamletea mawindo na kumtunza, na alikuwa mvulana mzuri. Mambo mengi ambayo waaminio wa kimwili hufanya katika mstari wa dini, kusaidia jamii, na—na kulipia watu bili za hospitali, na mambo ya kidini, lakini hilo silo ninalozungumzia.

36 Moabu alikuwa mzuri, taifa kuu, ndugu kwake. Naye Yakobo alikuwa amefanya kila kitu, alikuwa mwasi; lakini bado alikuwa na jambo moja la kufanikisha, hilo lilikuwa ni kupata ahadi hiyo, haki hiyo ya mzaliwa wa kwanza. Hapa inakuja Israeli, watoto wa Yakobo, wakiwa na lengo lile lile. Sasa ni nani atakayekuwa sahihi?

37 Balaamu alijenga madhabahu saba; katika Israeli kulikuwa na madhabahu saba. Balaamu alitoa dhabihu saba za wanyama safi; Israeli walitoa dhabihu saba za wanyama safi. Huko, mradi tu wanalichukulia kidesturi, Moabu walikuwa wa kidini kama vile Israeli walivyokuwa, Esau alikuwa wa kidini kama vile tu Yakobo alivyokuwa, na Kaini alikuwa wa kidini kama Habili. Lakini, ni uteuzi ndio unaoshikilia.

38 Kipofu jinsi gani! Jinsi upofu wa watoto wa Esau, tukinena kiroho, Wamoabu, waliwaangalia Israeli na kusema, "Waangalie. Wao si dhehebu. Wao ni kundi la waasi. Wanaishi katika mahema. Na sisi ni taifa kubwa. Walifanya uovu. Nao hawana shirika kati yao. Wanazunguka-zunguka tu, wakimfuata nabii." Lakini alishindwa kuona Nyoka wa Shaba na Mwamba uliopigwa ukienda mbele yao. Alishindwa kuona kundi hilo lililoitwa, lililochaguliwa likifuata utaratibu wa Kiungu wa Mungu kwa nchi ya ahadi.

39 Hivyo ndivyo ilivyo leo hii. Wanasema, "Ni kundi la watakatifu wanaojibingirisha. Ni kundi la watu ambao ni *hili, lile,* au *linginelo*." Lakini wanashindwa kuona kwamba ni kufuata mwongozo wa Neno la Mungu.

40 Israeli ilikuwa njiani kuelekea kwenye nchi ya ahadi. Mungu, katika Neno Lake, alitoa ahadi.

41 Yakobo, sababu ambayo alichagua kupata haki hiyo ya mzaliwa wa kwanza, bila kujali, alitaka kuipata, kwa sababu alijua kuwa haki hiyo ya mzaliwa wa kwanza ilishikilia baraka.

Ilishikilia uzima. Hakujali jinsi ilivyokuja, mradi tu aliipata. Hilo ndilo lililokuwa jambo muhimu. Kwamba imekuja kwa ndege gani, haikujalisha. Aliitaka. Na lazima awe nayo. Na aliipata. "Heri wale wenye njaa na kiu ya haki, watashibishwa." Alikuwa njiani mwake, na alikuwa akiifuata, na akaipokea.

42 Israeli ilikuwa njiani kuelekea nchi ya ahadi. Haijalishi ni Wamoabu wangapi na laana ngapi walijaribu kuweka juu yao, walikwenda moja kwa moja kwenye nchi ya ahadi.

43 Na leo hutawahi . . . haijalishi wanapata sheria ngapi, mashtaka kiasi gani, mateso kiasi gani, wanasema mambo maovu mangapi, ni mara ngapi wanaita "mtakatifu anayejibingirisha," ni mara ngapi wanasema mambo hayo mabaya, kanisa litaendelea. Halina budi kuendelea. Linadumu katika Neno la Mungu.

44 Wakati mmoja wafalme wawili walikuja pamoja. Mmoja wao alikuwa Ahabu, mbaya, yule mwingine alikuwa Yehoshafati; kanisa la kiroho, kanisa la kimwili.

45 Ahabu alikuwa mwaminio mkwamia mpakani. Alikuwa na manabii. Hawakuwa makafiri. Hawakuwa waabudu sanamu. Walikuwa manabii wa Israeli, lakini wote walifundishwa na kulishwa na kuvikwa na mfalme Ahabu. Ikawa kama mahali ambapo walikuwa na uungwaji mkono wote wa kisiasa.

46 Yehoshafati aliingia, akishuka, akafanya muungano, jambo ambalo si sawa.

47 Hupaswi kamwe kuungana na wasioamini. Hatupaswi kamwe, kwa njia yoyote, kuweka majina yetu kwenye vitabu katika makanisa ambayo hayaamini Injili yote. Hasha! Utapata shida.

48 Nao wakapata shida. Na mtu huyu mwadilifu akasema, "Je, haitupasi kumtaka Bwana shauri kwanza, na kujua ikiwa tunapaswa kwenda Ramoth-Gileadi?"

49 Sasa angalia jinsi mkao wa mambo ulivyoonekana mzuri. "Ramoth-Gileadi ni yetu. Ni mali yetu, na Washami wameichukua kutoka kwa Mungu aliye hai. Hivi hatutapanda kwenda na kuichukua nchi hii?" Naye akaifanya hotuba hiyo kuwa nzuri sana, na ya kisheria sana, na ya haki sana, mpaka Yehoshafati akaiangukia.

50 Na, leo hii, watu wanaweza kusimama kwenye mimbara wakiwa na akili kama hiyo na kutoa hotuba, na elimu, mpaka wanaweza kuelezea na kuondolea mbali Nguvu za Roho Mtakatifu kwenye Biblia. Wanaweza kuondolea mbali uponyaji wa Kiungu kwa maelezo. Wanaweza kuondolea mbali kunena kwa lugha na tafsiri kwa maelezo, wanaweza kuelezea ubatizo wa Roho Mtakatifu, hadi siku nyingine.

51 Lakini mtu aliyeteuliwa na Mungu, mtu . . . "Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu." Una uteuzi huo wa Mungu juu yako, hautakukwaza kamwe.

52 Yehoshafati alisema, mfalme mwenye haki alisema, "Je, hakuna nabii, hata tuweze kumtaka Bwana shauri?" Ahabu alikuwa akiendelea bila hiyo.

53 Hivyo ndivyo kanisa la kimwili linavyofanya siku hizi. Loo, wana seminari zilizojaa wahubiri, watu mashuhuri, maprofesa mashuhuri, wasomi, werevu, wenye akili, loo, jamani, mbali zaidi ya a—akili za kanisa la kawa- . . . au kanisa la kiroho.

54 Katika siku za Nuhu, katika siku hizo, angalia kanisa la kawaida. Walikuwa nini? Wanasayansi, wajenzi, watu werevu. Lakini wateule, Henoko na Nuhu, walikuwa wachungaji na wakulima, wanyenyekevu, wasio na elimu, wasio na akili, lakini walimjua Mungu wao; kitu ndani yao, kikisonga, kikiita. Tutafikia hicho baada ya kitambo kidogo.

Sasa, kwa hiyo Yehoshafati akasema, "Hivi hakuna nabii?"

55 Loo, kwa kweli, wa kimwili anao. "Hakika, tunao. Ninayo seminari hapa chini, iliyojaa hao."

56 Akaleta mia nne. Sasa, hawa sio makafiri. Ni waabudu wa Yehova-Mungu. Wakaja, nao wakasema, "Wacha tuwe na muda kidogo ndipo tutatabiri." Na kwa hivyo wote walikusanyika pamoja. Na wakarudi na, "Neno la Bwana," na wakasema, "BWANA ASEMA HIVI." Manabii wa Israeli. "BWANA ASEMA HIVI. Kwea, Bwana yu pamoja nawe. Na utachukua Ramoth-Gileadi, kwa sababu kwa kweli ni mali ya Israeli." Na mmoja wa wanaume wakuu akamtengenezea pembe mbili kubwa kutoka kwa chuma, kama mwakilishi, na akaenda kusukuma. Akasema, "Kwa hizi utawasukuma Israeli . . . au kuwasukuma Washami mbali na Ramoth-Gileadi."

Lakini, Yehoshafati, kitu fulani ndani yake!

57 Loo, natumai kuwa Mungu ataliweka jambo hili moyoni mwako. Si kitu ambacho unaweza kupata kwa kujielimisha. Sio kitu ambacho unaweza kujiingiza kwa kusoma. Ni kile ambacho Mungu, kwa uteuzi, anakufanyia. "Si yule akimbiaye au yule aonyesha- . . . Ni Mungu anayeonyesha rehema."

58 Yehoshafati akasema, "Ni wanaume waliovalia nadhifu." Hapana shaka alisema kitu kama hiki, "Wao ni wenye akili, na wanaume werevu kuliko wote ambao nimewahi kusikia. Wameelimika hadi sasa. Msimamo wao ni umoja. Wana umoja mkubwa kati yao. Nao ni werevu, na wana Ukweli mwingi kwao."

59 Makosa yote yana Ukweli. Uongo mkubwa uliowahi kusemwa ulikuwa na tisini- . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] asilimia ya Kweli ndani yake, uwongo ambao Shetani alimwambia Hawa.

60 "Loo, ni Ukweli mwingi katika kile wanachosema, lakini je, hakuna mmoja zaidi?"

61 Vema, unafikiri mtu huyo alisema nini? "Wakati tukiwa na mia nne hapa, werevu kuliko wote, walio bora kuliko wote? Hawako hapa nje jangwani wakikimbia karibu nusu uchi, na huku wamejizungushia ngozi ya kondoo, au kitu kingine. Ni wanaume ambao nimewalisha, nimeelimisha. Sio wanaume ambao hawajui ABC zao. Wao ni wasomi, na wanajua jambo hilo. Wanakaa, mchana na usiku, wakisoma magombo na unabii. Wanajua kilicho sahihi. Ninao tayari. Na wamesimama hapa kwa nia moja, mia nne wao, wakisema, 'Kwea, Bwana yu pamoja nawe.'"

62 Lakini ikiwa ningeweza kusoma mawazo ya Yehoshafati dakika chache, "Kuna kitu tu ambacho hakiingii," angeweza kusema. "Kuna kitu tu ambacho hakionekani kuwa sawa. Hivi hakuna mmoja tu zaidi, mahali fulani?"

63 "Loo," akasema, "ndiyo, kuna mmoja zaidi, lakini yeye si wa shirika. Yeye ni jamaa wa aina tofauti. Yeye ni haini tu." Yeye ni kama Yakobo. "Lakini tunaweza kumuuliza. Wanasema yeye ni nabii. Lakini nina shaka na hilo, kwa sababu yeye kila wakati ananilaani, akisema kwamba *hili, lile,* au *linginelo*, au hatabiri mema kamwe juu yangu." Angewezaje? Unaona?

64 Basi wakasema, "Twende tukamchukue. Yeye ni mwana wa Imlah." Basi wakaenda wakamchukua.

65 Na mtu fulani alikutana naye barabarani, akasema, "Sasa, wewe sema kitu kile kile wanachosema. Lazima ukubaliane na chama. Usipofanya hivyo, ole wako!"

66 Akasema, "Nitasema tu kile Mungu atakachoweka kinywani mwangu kusema, na si kitu kingine chochote."

67 Halafu baada ya kufika huko, na wakampa usiku mmoja, alisema, "Kwea, lakini niliona Israeli wametawanyika kama kondoo wasio na mchungaji."

Naye Ahabu akasema, "Si nilikuambia?"

68 Sasa, kuna mia nne dhidi ya mmoja. Wanaume mia nne waliofunzwa, werevu, walioelimika, wenye akili dhidi ya mjinga mmoja mdogo, kama vile tungemwita, Mikaya. Mtu mmoja, lakini hata hivyo mtu huyo mmoja alikuwa na Neno la Bwana, hiyo ilileta tofauti. Kila moja yao ilikuwa ya uwongo, ilithibitika kuwa ya uwongo. Kwa nini Mikaya alikuwa tofauti sana? Je, ilimbidi kuwa maskini, awe tofauti? Hapana. Ninii... Kilichomfanya Mikaya awe tofauti, alidumu na Neno. Neno la Mungu ndilo alilokaa nalo.

69 Sasa imeahidiwa kuwa, katika siku hizi, "Mungu atamwaga Roho Wake." Imeahidiwa na Daniel, kwamba, "Watu, katika siku ambazo jiwe litapiga ile sanamu kwenye mguu, watu wanaomjua Mungu wao watatenda mambo makuu." Unabii baada ya unabii!

Na seminari zote, ulimwengu, haziwezi kuichukua. Mungu ataifanya, kwa vyovyote vile, na watu wataifuata. Unaona? Wa kimwili na . . . Kanisa la kawaida na kanisa ka Kimbinguni. Unaona, Neno huleta tofauti.

70 Hiyo ndiyo Yakobo aliyofikiria, "Na haijalishi ni nini, najua siwezi kubarikiwa kamwe isipokuwa niishike haki hiyo ya mzaliwa wa kwanza. Haki hiyo ya mzaliwa wa kwanza ndiyo itakayonilazimu kupata."

71 Pia, lakini Esau aliichukia, na watoto wake wanafanya hivyo hivyo, bado, hata wa leo. Wanaichukia. Daima imekuwa hivyo.

72 Wakati wowote kunapokuwa na uamsho, kila wakati huzaa mapacha. Hilo ni tamshi fidhuli, lakini ni kweli. Wakati kulipokuwa na uzazi kutoka kwa, kutoka kwa Isaka na Rebeka, ulizaa mapacha. Ulimwengu ulipoumbwa, ulizaa mapacha, miti miwili. Na wakati Kaini na Habili walipozaliwa, ilizaa wawili. Wakati Ishmaeli na Isaka walizaliwa, ilizaa wawili. Na wakati Esau na Yakobo walizaliwa, ilizaa wawili. Mmoja wao, wa kawaida (mmoja wao, wa duniani); huyo mwingine, wa Kimbinguni. Na mmoja aliangalia wa kawaida, mwenye akili; yule mwingine alitembea kwa Roho. Imekuwa hivyo kila wakati. Wakati kanisa la Kilutheri lilipotokea . . .

73 Wacha tuchukue Pentekoste, kwanza. Angalia kuzaliwa kwa Pentekoste. Ilileta uamsho mkubwa, wenye nguvu ambao uliufagia ulimwengu unaojulikana, Pentekoste. Haikuchukua muda mrefu baada ya Pentekoste hata Paulo akasema, kwamba, "Kutakuwa na wanaume watakaoinuka kati yao, na vitu vya kupotosha, na watawafanya watu wamwache Mungu." Na hivyo ndivyo hasa walivyofanya. Inazaa wawili.

74 Wakati kanisa la Kilutheri lilipozaliwa, Martin Luther alileta uamsho wa kiroho. Haikuwa muda mrefu sana mpaka hapa alipokuja Esau, moja kwa moja nyuma yake, na kuiundia dhehebu. Na ilitoa wawili.

75 Halafu baada ya hapo, akaja Mmethodisti, John Wesley, uamsho wa kiroho. Na baada ya hapo, likaja shirika, likaunda dhehebu. Na ilitoa mbili.

76 Na baada ya hapo, ikaja Pentekoste, uamsho. Na sasa wameiwekea utaratibu, na sasa wanatulia kwenye dhehebu. Nayo inazaa mbili.

77 Lakini ule uzao wa kiroho wa Mungu aliye hai, ingawa lazima awe mgeni, ingawa lazima awe mzururaji, daima husababisha utengano. Esau hakudumu sana na Yakobo. Mara tu Yakobo alipopata haki ya mzaliwa wa kwanza (Mungu asifiwe), ilihitaji utengano. Na wakati mtu . . . Sijali wewe ni wa kanisa gani, ikiwa ni la kimwili, na wenzako unaoshirikiana nao, watu unaocheza nao karata, na vyama vyako vya fasihi, na kadhalika; unapopata haki ya mzaliwa wa kwanza, kitu ambacho kiko chini moyoni mwako ambacho kinamwonea

Mungu njaa, unapopokea hiyo, inahitaji utengano. "Tokeni miongoni mwao, mkatengwe, asema Mungu." Utengano!

78 Kanisa linatulia. Unaona, haliwezi kuendelea. Esau alikuwa mfano mzuri sana wa mwaminio wa kimwili leo, asiyeweza kuushinda ulimwengu. Yeye hashindi mambo ya ulimwengu. Bado wanapenda karamu zao za ulevi, kucheza kwao dansi, vipodozi vyao vya kujipamba na, wanawake, kwenye nyuso zao, na—na kukata nywele zao na—na kuvaa maskini hizi nguo fupi; na—na wanaume wanapenda kwenda kwenye vyumba vya kucheza kamari, na—na kuvuta sigara, na kufanya mizaha midogo michafu; na bado ni washirika wa kanisa. Hawawezi kamwe kushinda vitu hivyo. Wala Esau hakuweza. Lakini hata hivyo, kuwa wa kidini, ilibidi atulie kwenye wazo la kiakili. Hilo ndilo jambo lile lile kanisa linalofanya leo. "Tutakuwa shirika. Tutajiweka pamoja. Tutafanya ukoo, au kikundi, au kitu kama hicho."

79 Na hivyo ndivyo kanisa linavyotembea leo, wa kiroho na wa kimwili, bado ni sawa. Haijabadilika, na kamwe haitabadilika.

80 Utakatifu wa Mungu. Mungu, akiwa Mungu, anaonyesha hilo, Mwenyewe. Ikiwa hakungekuwa na mwenye dhambi, hakungekuwa kamwe . . . Asingeweza kuwa Mwokozi kamwe. Lakini alikuwa Mwokozi mwanzoni, kwa hivyo hakukuwa na kitu kilichopotea. Na sifa Zake Mwenyewe kuwa Mwokozi, zilileta mwenye dhambi, ilibidi kuwe na kitu cha kuokolewa. Kabla ya kuwa na kitu chochote kilichookolewa, ilibidi kuwe na kitu kilichopotea. Na haki Yake na utakatifu Wake! Ikiwa hakukuwahi kuwa na m—mtu mgonjwa, asingekuwa mponyaji hata. Lakini tangu mwanzo, na kuhusu mianzo, Yeye alikuwako kabla ya mwanzo. Alikuwa mponyaji. Kwa hivyo hakukuwa na kitu chochote kigonjwa, kwa hivyo ilidhihirisha mtu mgonjwa, ili aweze kuwaponya, kumfanya Yeye kuwa mponyaji.

81 Kutoka katika Eneo lile lile Takatifu kulikokuja wokovu, kulikuja laana. Kutoka kwa mama na baba wale wale waliomzaa Yakobo, walimzaa Esau. Unaona? Ni Mungu. Hawezi kubadilisha mpango Wake. Lazima waende vivyo hivyo tu. Maumbile yote yatatoshea katika huo. Hayana budi. Mnapata ninalomaanisha? Huyaingiza moja kwa moja. Lazima kuwe na mtu aliyepotea, kuokolewa. Na ikiwa hakungekuwako, Yeye, ninii Yake . . . Yeye akiwa Mwokozi alifanya hivyo. Kilindi kinaita Kilindi.

82 Kama yule mvulana mdogo ambaye mimi huzungumza juu yake kila mara, kula vifutio kutoka kwenye penseli, na pedali kutoka kwenye baiskeli, alihitaji salfa. Na mradi tu kulikuwa na kitu ndani humo kinachotamani salfa, ilibidi kuwe na salfa mahali fulani, kwanza, iliyotengenezwa. Ilibidi kuwe na salfa kabla ya yeye kuwa na shauku hiyo. Na hiyo, salfa, ilimleta, kisha akarudi kwenye salfa.

83 Hiyo ndiyo njia ambayo Mungu ni Mwokozi. Na ilibidi kuwe na kitu kilichopotea, ili Yeye aokoe, ili kumfanya Yeye Mwokozi. Hayo ndiyo yote inayofanya, yanaonyesha Mungu. Kila kitu, vyote viko ndani Yake; si ndani ya mhubiri, si ndani ya kanisa, si katika shirika, lakini katika Mungu, ili uteuzi uweze kusimama kikamilifu. Unaona? Iko ndani Yake. Ndiyo. Ninii ya kilutheri . . .

84 Halafu tunaona utengano mwingine, huyo alikuwa ni Ibrahimu na Lutu. Walikuwa ndugu. Lakini Lutu alikuwa mwenye mawazo ya kimwili. Siku zote alikuwa akitafuta kitu kikubwa, kitu kilicho na mapambo mengi juu yake. Kama tu nyani, kama vile ningesema, kila wakati akitafuta kitu kinachong'aa. Roho hiyo haijawaacha watu, leo. Watatafuta . . . Wanaenda mjini, na hawatakuja kwenye kibanda kidogo kama hiki. Unaona? Wanataka kanisa kubwa kuliko yote lililoko mjini, mchungaji msomi kuliko wote, ambapo watu waliovalia vizuri zaidi huenda, ambapo meya huenda, kwenda mjini. Bado ni ile roho ya Esau. Kweli walikuwa na haki za mzaliwa wa kwanza, kwa kuanzia, wanajiita Kanisa, lakini wanaipoteza kwa sababu wanaidharau. Huwezi kuwafanya watu hao wapige magoti, na kulia na kumwomba Mungu, na kutoka nje na kufanya ibada ya uponyaji, na kuvumilia mateso ya ulimwengu, wampokee Roho Mtakatifu. Na wao—wao hawatafanya hivyo. Wanaidharau. Wanaiita "kundi la watakatifu wanaojibingirisha." Vile tu Biblia ilisema wangefanya. Wanafanya hivyo kwa sababu hiyo ndiyo asili yao. Ni asili. Kama vile kunguru na hua, asili mbili. Wanatamani kwa sababu ndivyo walivyo. Hawatawahi (kamwe) kuona mwingine, kwa sababu hawakuzaliwa kuona hiyo.

85 Na yule mwingine, usingeweza kumzuia na hiyo, kwa sababu ni uteuzi wa Mungu. Amezaliwa kuwa mwanamume wa kiroho au mwanamke wa kiroho. Kitu ndani yake kinaionea shauku. Loo, na—natumaini hii inafika mahali ambapo tunaweza, mnaweza kuona kile ni—ninachomaanisha, kwa kuihitimisha sasa. Sasa Ibrahimu . . .

86 Kumbuka, mradi walishirikishwa pamoja, kanisa la kawaida na kanisa la kiroho, hawakupata baraka kamwe. Yakobo hakubarikiwa kamwe mpaka alipojitenga na Esau. Na Ibrahimu hakubarikiwa kamwe mpaka alipojitenga na Lutu.

87 Lutu alikuwa na mikutano yake midogo ya maombi kanisani kwake kule chini, aliwafundisha wanawe na binti zake, na hao wengine. Lakini aliishi maisha hivi kwamba, hata, alipoanza kuzungumza juu ya mwisho wa wakati, walimcheka.

88 Vivyo hivyo leo hii! Unazungumza juu ya uponyaji wa Kiungu na nguvu za Mungu, na kadhalika, wanaicheka. Ni roho ile ile. Hizo ndizo roho mbili kuu, kidini, ambazo zimeshika ulimwengu; mwaminio na asiyeamini, mwaminio na

anayejifanya mwaminio, mmoja anamwiga yule mwingine. Sasa wakati Ibrahimu alipojitenga . . .

89 Je, ulimwona Yesu? Katika kuzungumza Kwake juu ya Kuja, Kuja mara ya pili, Alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, watakuwa wakila, wakinywa, wakioa, na kuolewa." Lakini alipozungumza juu ya siku za Lutu, Yeye hakusema chochote juu yake. "Kama siku za Lutu," hiyo ni kwa ufunuo.

90 Angalia kile kilichotokea katika siku za Lutu. Kulikuwa na Lutu kule Sodoma, amekaa vizuri, kiakili, akawa ninii, mmoja wa watu wakubwa wa jiji, mwamuzi, aliyekaa malangoni na kuwahukumu watu. Mkewe alikuwa katika mashirika yote ya jiji hilo. Na binti zake, na wote, waliolewa kati ya watu mashuhuri, wasomi, wenye elimu ya juu, werevu, wenye akili. Naye Ibrahimu aliishi katika hema chini ya mti wa mwaloni. Lakini siku moja wote wawili walitembelewa.

91 Na kulikuwa na mhubiri mwenye akili aliyeenda huko chini akahubiri, na kuwaita watoke. Angalia—angalia ujumbe, "Toka," akamwambia Lutu.

92 Na hangeitwa kamwe ikiwa haikuwa kwa rehema ya Ibrahimu. Alisema, "Je, ninaweza kupata watu hamsini, utauacha? Je, ninaweza kupata watu thelathini? Naweza . . . Ikiwa nitapata kumi?" Huo ndio umbali alioweza kwenda. Na hakuweza kupata hata kumi kati yao.

93 Si ajabu, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu." Kumbukeni, Nuhu hakuwa mfano wa Kanisa; Henoko alikuwa, ambaye hakupitia kwenye dhiki, bali alihamishwa kabla ya dhiki kuanza. Henoko alienda Nyumbani, hakupitia kwenye dhiki. Nuhu alipitia.

94 Sasa, angalia kwa makini sasa tunapoingia katika hili. Angalia ni aina gani ya ishara ambayo Ibrahimu na familia yake walipata. Walipata ya Kimbinguni. "Ibrahimu!" Alijuaje kuwa alikuwa ni Ibrahimu? "Yuko wapi Sara, mkeo?" Alijuaje kwamba alikuwa ameoa, au alikuwa na mke, Sara?

"Yuko hemani."

95 Sasa, Mtu mmoja ameketi pale, akila nyama, akinywa maziwa, na akila ugali wa mahindi. "Wapi, yuko wapi Sara, mkeo?" Alijuaje jambo hilo? Alilijuaje? Wazia hilo. Unaita . . . Enyi watu wa kiroho, wacha hii iingie ndani yenu. Alijuaje hilo, wakati Yeye alifanya kama mgeni, vumbi kwenye nguo Zake?

Na Ibrahimu aliposema, "Yuko hemani, nyuma Yako."

96 Ndipo Yeye akasema, "Ninaenda . . . " "Mimi, mimi," kiwakilishi nafsi. "Mimi," Mtu huyu, Mungu akijitambulisha Mwenyewe katika mwili. Mungu! Ibrahimu alimwita Elohimu. "Mimi, nitakutembelea. Nitatimiza ahadi Yangu. Na kulingana na wakati wa uhai, nitakutembelea, na utampata mvulana huyu

ambaye niliongea nawe habari zake." Naye Ibrahimu, mia; Sara, tisini.

97 Na Sara, nyuma kule hemani; karibu mahema manne madogo, hema kuu limewekwa huko nyuma. Nyuma ya mapazia, alikuwa akisikiliza. Alisikia. Na chini moyoni mwake alitabasamu, akasema, "Mimi, mwanamke mkongwe wa miaka mia moja, na bwana wangu," mume wake, "bwana wangu, na mkongwe, na kufikiria kuwa tutakuwa na raha pamoja tena, kama vijana waliooana? Loo, inawezekanaje?" Na yeye kwa namna fulani akatabasamu.

98 Alikuwa ameelekeza mgongo Wake kwenye hema. Akasema, "Kwa nini akacheka?" Loo, ndugu, wewe hapo!

99 Angalia kanisa la kimwili linalohubiriwa Injili. Billy Graham wa kisasa na hao wengine kule chini wakihubiri Injili, "Toka ndani yake!" Lakini je, walitoka? Hapana. Wachache sana, sana, sana.

100 Angalia kundi la Ibrahimu, walioitwa watoke. Sasa angalia. Naye akampa ishara hii, naye akamwamini. Ndipo akatoweka mbele zake, akaenda zake. Loo, jinsi imekuwa ni kujitenga kila mara, walioitwa watoke!

101 Sasa, roho hizi mbili. Kuharakisha na wewe, kuharakisha sasa kufika mahali pangu ninapotaka uone. Vikundi hivi viwili vimekuwa vikishirikiana kwa karibu, kote katika nyakati, tangu mwanzo hasa wa wakati; kanisa la kawaida, kanisa la kiroho. Wamepitia Agano la Kale, walikuwa kupitia Agano Jipya, na wangali chini hata wa leo.

102 Sasa, yapata miaka elfu mbili iliyopita, ilifikia upeo, na ikaongozwa na wanaume wawili: mmoja wao, Yesu Kristo; yule mwingine, Yuda Iskariote. Sasa, Yesu alihusisha Kuja, kwa Kuja Kwake mara ya pili, kwamba hizi roho mbili zingekuwa tofauti sana na kile walichokuwa huko nyuma. Sasa hapa ndipo ninapotaka uweke mavazi ya—yako ya Utukufu. Roho hizi mbili zitakuwa tofauti. Kwa sababu, Shetani alikuja na kuishi ndani ya mtu ambaye alikuwa mshirika wa kanisa, Yuda Iskariote, aliishi katika kanisa la kimwili, na alikuwa rafiki wa kanisa wakati wote. Lakini aliingia na—na kudanganya, au kudhani alikuwa akimdanganya ndugu yake. Aliingia na akahesabiwa kuwa ni mmoja wao; akaonja mazuri ya Mungu, akatembea moja kwa moja katika Roho, alivyoonekana kuwa, akatoka na kuhubiri Injili, na kutoa pepo. Lakini chini ndani yake, wakati wote, yeye alikuwa Yuda, kwa kuanzia. Biblia ilisema, "Alizaliwa mwana wa upotevu."

103 Sasa kumbuka, kuna kanisa la kimwili huko nyuma, Esau, Mafarisayo na Masadukayo.

104 Lakini mwangalie jamaa huyu anayejifikiria kuwa tu. . .Atatembea pamoja na Ujumbe kwa muda, lakini hataki tu kuweka mikono yake juu Yake kupita kiasi.

Unaona hizo roho? Yesu alisema, “Litakuwa karibu sana na kitu halisi, litawadanganya Wateule hasa,” Wateule, kama utaangalia, “kama ingewezekana.” Lakini haiwezekani. Unaona, itadanganya.

105 Sasa angalia, sio tu kanisa la kimwili, moja huko nje, kanisa la kawaida la kidesturi, kundi la Esau.

106 Tulipata sasa kundi la Yuda, ambalo ni la hila zaidi, lenye hila zaidi, likija moja kwa moja kwenye mikono hasa ya baraka. Kama vile tu katika Waebrania 6 na 10, jinsi alivyosema, “Mara baada ya kufanywa washiriki na kuonja nguvu za ulimwengu ujao, na wamefanya mambo haya yote; kama . . . na kisha ikiwa wamepokea ujuzi wa Haki, na ndipo ikiwa watajiondoa makusudi.” “Makusudi,” hiyo ni nini? “Kuhesabu Damu ya agano, ambayo walitakaswa nayo, kitu kiovu.”

107 Hebu niwape mfano. Huu hapa. Huyu hapa mtu, yeye ni jamaa mzuri, mvulana mzuri. Ameitwa, anahisi moyoni mwake anataka kuwa mhudumu. Vema, anamkubali Yesu kama Mwokozi wake binafsi. Yeye ni mvulana mzuri, hakuna mtu anayeweza kusema chochote dhidi yake. Baada ya muda, mada ya utakaso. Mtu huyo anashikwa na tamaa mbaya akiwatazama wanawake. Yeye . . . Iko ndani yake. Unaona? Halafu, jambo linalofuata, labda alivuta sigara, na anataka kuvuta sigara. Labda anataka kucheza kamari. Labda anataka kufanya jambo baya. Anajua hapaswi kufanya hivyo, kwa hivyo anasema, “Ee Mungu, iweke Damu ya Yesu kwangu, na unitakase.”

108 Naye anatakaswa. Anaweza kupaza sauti, kumsifu Bwana, kufanya mambo kadhaa, pia, kwenda nje na kufanya jambo. Kumbuka, Yesu alisema aina hiyo watakuwapo siku hiyo. “Wengi watakuja na kusema, ‘Bwana, hivi sikutabiri, nikahubiri? Hivi sijatoa pepo, kwa Jina Lako?’” Yesu alisema, “‘Hata sikukujua, ewe mtenda maovu.’” Unaona, hao hapo.

109 Sasa angalia hili sasa. Tunakuja kutengeneza moja juu ya milioni mia moja ya unywele, moja kwa moja kufikia makali ya Injili, “Kali kuliko upanga ukatao kuwili, unakata hata kugawanya mfupa, na Mtambuzi!” Haleluya! Mungu, acha ipite. “Mtambuzi wa mawazo ya moyo.” Hiyo ni Injili, Nguvu za Mungu. Neno la Mungu lililodhihirishwa ndilo Injili.

Unasema, “Biblia ilisema. Hilo ni—hilo ni Neno la Mungu.”

110 Vema, Neno lililodhihirishwa ndilo Injili. Injili ilitujia si kwa njia ya Neno tu, bali kwa nguvu na madhihirisho ya Roho Mtakatifu, kuonyesha Nguvu, kufanya Injili iishi.

111 Nilipokwenda India, askofu mkuu wa—wa kanisa la Methodisti alijitokeza, akasema, “Bw. Branham, hatutaki kujua chochote juu ya mmishenari. Tunajua mengi juu ya Biblia kuliko vile nyote mtakavyowahi kujua.” Kasema, “Tulikuwa kanisa, na tukakaa hapa miaka elfu mbili kabla ya nyinyi kuwa taifa.” Hiyo ni kweli. Lakini akasema, “Tunasikia kwamba

Mungu amekutembelea na amekuletea karama ambayo inaweza kuifanya Biblia hii kuishi." Akasema, "Hiyo ndiyo tunayovutiwa nayo." Loo, jamani! Tazama, mtu huyo alikuwa mwana, sio mjukuu, kama Daudi alivyosema. Unaona? "Tunataka kujua. Ni kweli?"

112 Nikasema, "Hakika, ni kweli. 'Yesu Kristo yeye yule jana, leo na hata milele.'"

113 Sasa, mwangalie, kanisa la kawaida likilitesa kanisa la kiroho. Sasa, tunaona basi kwamba Yuda alijifanya kuwa ndugu, ndugu, na kisha akainuka na mwishowe akafikia kilele.

114 Sasa mwangalie huyu mhubiri kijana. Anafikia mahali, anasema, "Bwana, nimekuwa nikiangalia wanawake. Sipaswi kufanya hivyo. Nimekuwa, unajua, kwa njia fulani nafanya mambo ya ulimwengu. Sipaswi kufanya hivyo. Nimekuwa nikitumia pesa zangu kwenye mbio za farasi. Si—sipaswi kufanya hivyo. Ni—nimekuwa nikienda kila usiku kwenye sinema. Sipaswi kufanya hivyo. Ninafurahia hata picha za uchafu na vitu kama hivyo, nina picha zilizobandikwa kwenye chumba changu. Sipaswi kufanya hivyo. Hayo ni mambo ya ulimwengu. Nitakase, Bwana!"

115 Bwana akasema, "Sawa, nitafanya hivyo." Yeye anatumia Damu ya Yesu Kristo na kumtakasa.

116 Halafu, wakati anapofanya hivyo, usiku mmoja hupita na anasikia kitu. Anaenda na kusikiliza. Yeye husikia juu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, kujazwa na Roho. Kisha anaangalia ndani yake, "Loo, jamani, hiyo si ni ajabu! Lakini, tuseme, hiyo ingeharibu huduma yangu ikiwa ningeihubiri hiyo. Hiyo ingemfanya mama kunitorosha nyumbani. Wangeweza kuniondoa kutoka kwa kanisa langu ikiwa ningewahi kwenda kwenye hiyo. Loo, afadhali niachane na hayo. Lakini wacha niiangalie. Naam, hiyo ni Kweli, Biblia."

117 Vema, kama mhudumu fulani mashuhuri, anayejulikana ulimwenguni kote, alipatikana hivi majuzi (na mtu ambaye alikuwa pamoja nami huko Puerto Rico) akiwa amepiga magoti, akinena kwa lugha, huko London, Uingereza; mtu mwenye nguvu, mmoja wa wainjilisti wakuu kuliko wote ulimwenguni leo. Na mtu huyu, ndugu yake akiwa pamoja nami hapa, mtu aliyejazwa Roho, akamkimbilia na kusema, "Loo, ndugu, jambo ndilo hilo."

118 Akasema, "Ninaijua. Ninaijua. Lakini, angalia, hebu niwaambie jambo fulani."

119 Akasema, "Ihubiri sasa. Ihubiri. Hii ndiyo saa. Kwa ushawishi wako, ungeweza kuutikisa ulimwengu."

120 Akasema, "Hapana, siwezi kuihubiri. Unaona, ka—kanisa lingenikataa. Nisingeweza kuhubiri hayo. Singeweza kuifanya." Loo, ndugu!

121 "Mmepo-. . .mkiisha kutakaswa na kuja kupokea ujuzi wa Kweli, mkaingalia, na kuona kuwa ni kweli; na kuiacha, kwa kuwa wanamsulubisha Mwana wa Mungu kwao wenyewe, na kumtia aibu wazi wazi, wakiionea aibu Injili."

122 Paulo alisema, "Siionei aibu Injili ya Yesu Kristo, kwa maana ni Nguvu za Mungu kwa wokovu." Ni Nguvu za Mungu zinazofanya kazi miongoni mwa Kanisa Lake.

123 Lakini wakasema, "Nisingeweza kufanya hivyo." Mtu huyu akasema, "Wangeweza kufikiria mimi ni mpentekoste. Wangenifanya mimi. . . " Akasema, "Si—sifa yangu ingeharibiwa." Loo, ndugu!

124 Sina sifa yoyote. Ninafikiria juu ya Yake. Sifa Yake, huyo Ndiye.

125 Lakini angalia jinsi wanavyoweza kuja karibu Nayo, unajua, "Na kuhesabu Damu ya agano aliyotakaswa nayo, kitu kilichomtakasa na kumtoa ulimwenguni, na kujaribu kumweka Hapa ndani. Halafu yeye hukiangalia Hicho, na ana ujuzi Nacho. Kukiacha Hicho, haibaki dhabihu tena kwa ajili ya dhambi," Biblia ilisema, "ila kuangalia kwa kutisha kwa hukumu na ghadhabu ya moto inapaswa, itaninii, itakayomwangamiza mpinzani. 'Kwa maana kulipiza kisasi ni kwangu,' asema Bwana. Yeye ambaye alidharau sheria ya Musa, alikufa bila huruma, chini ya mashahidi wawili au watatu. Ni adhabu zaidi jinsi gani, na adhabu kali zaidi, ingawa inastahili, mhudumu ambaye amekanyaga Damu ya Yesu Kristo chini ya miguu yake, baada ya kupokea ujuzi wa Kweli, na akaihesabu kuwa si kitu kitakatifu." Whwi!

126 Unaona mahali tulipo? Yesu alisema, "Kuwa mwangalifu." Unaona jinsi Yuda alivyokuwa? Alikuwa moja kwa moja pamoja nao. Yeye ndiye Esau, aliyekuzwa zaidi kwa ajili ya wakati huu. Alikuwa mdanganyifu, mwigaji, aliyekuzwa zaidi kwa ajili ya wakati huu. Hapa alikuja moja kwa moja, tena, kwa ndugu yake Yesu, ndugu aliyejifanya. Lakini moyoni mwake, alikuwa pamoja na kanisa la zamani la kimwili wakati wote, kwa sababu hapo ndipo alipomuuzia Yesu. Alimuuza Yesu, haki yake ya mzaliwa wa kwanza, kama vile tu Esau alivyofanya kwa ajili ya mlo wa dengu. Aliuza haki yake ya mzaliwa wa kwanza kwa vipande thelathini vya fedha.

127 Wanaume na wanawake wengi leo wameuza haki yao ya mzaliwa wa kwanza ya kiroho kwa umaarufu fulani, kitu kidogo cha ulimwengu hujawahi kushinda; kitu kidogo, wanawake, kujipodoa na kukata nywele, kuvaa nguo fupi; wanaume, kwa maskini mzaha mchafu na kuvuta sigara, kitu cha ulimwengu. "Ikiwa unapenda ulimwengu au vitu vya ulimwengu, upendo wa Mungu hauko ndani yako," ilisema Biblia.

128 Sitaki kuwaudhi, lakini tuko hadi mwisho. Tunakuja sasa, tunapanda ngazi haraka sasa.

129 Unaona jinsi ilivyo? Wanafanya hivyo. Wamekusudiwa kimbele. Wanaweza kuiga na kuwa wazuri na wanyenyekevu, karibu tu, kama Wakristo, karibu sana ambayo ingewadanganya Wateule hasa; lakini kwa matunda yao mtawatambua.

130 Mwanamke aliyevaa kaptura, hakuonekana kamwe kama Mkristo kwangu mimi. Biblia ilisema, "Ni jambo la dhambi na la aibu kwa mwanamke kukata nywele zake." Ni mwanamke mmoja tu katika Biblia aliyewahi kupaka uso wake rangi, alikuwa Yezebeli.

131 Vipi kuhusu wanaume, ninyi wanaume ambao mnadhaniwa kuwa wanaume Wakristo, na kuwaruhusu wake zenu kufanya hivyo? Wakati, Mungu atawawajibisha kwa hilo! Sio mtu! Mwili! "Loo, nitatoka basi na nijiunge na kanisa hili." [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] " . . . unafikiria juu yake." Hiyo ndiyo hasa kabisa yale Maandiko yaliyosema wangefanya, na hivyo ndivyo hasa walivyofanya. Na hivyo ndivyo watakavyofanya, kupatana!

132 Mtu fulani alisema, "Billy, ikiwa hutaacha hilo, utamtorosha kila mtu."

133 Kuna Kitu kimoja ambacho hakitaenda, Roho Mtakatifu, kwa sababu Hicho ni Neno Lake. Na mwaminio halisi aliyekusudiwa kimbele hataondoka, kwa sababu Hicho ni Chakula kwa nafsi yake. Anakipenda. Hakuna kitu kinachoweza kumweka mbali na Hicho. Atafanya chochote, kama Yakobo, lakini anataka haki hiyo ya mzaliwa wa kwanza. Atasimama pale. Sijali ikiwa inagharimu kila rafiki aliye naye, ikiwa inagharimu kazi yake, ikiwa inagharimu ushirika wake wa kanisa, ikiwa inagharimu kila kitu. Bado atashikilia, kwa sababu hawezi kujizuia. Kuna kitu ndani yake, kinachomsukuma, kilindi kinaita Kilindi. Loo, haya basi, kitu ndani yake!

134 Angalia, chochote unachotaka kupata ndani ya Biblia, na ukichukue hapa, rudi kwenye Mwanzo na uone mahali kilipoanzia, uone mahali kimefikia. Roho zote na harakati leo zinarudi kwenye Mwanzo. Ndivyo tulivyofanya, kuwathibitishieni mambo haya mnayoyaona, marafiki. Usisahau hiyo. Usiruhusu ipite juu ya kichwa chako. Acha izame ndani yako. Hayo ni mambo ya Mungu. Ilifikia kwenye kichwa; na Yesu alitabiri kwamba ingefikia kwenye kichwa tena katika siku za mwisho, na itakuwa kwa hii: Muhuri wa Mungu, na alama ya mnyama; nguvu mbili za kiroho zinazofanya kazi pamoja.

135 Sasa, mtu yeyote anajua ya kwamba Muhuri wa Mungu ndio haki ya mzaliwa wa kwanza, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Waefeso 4:30, inasema, "Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwaye mmetiwa muhuri hadi siku ya ukombozi wenu." Wakati walipozaliwa mara ya pili, walijazwa na Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu ni Kuzaliwa upya, tunajua hilo.

Ume—umechukuliwa mimba na Roho, nitakubali hilo. Lakini mpaka uzaliwe!

136 Kuna mtoto amechukuliwa mimba ndani ya tumbo la mama yake, ana maisha ya aina moja. Hayo ni maisha, na maskini ninii yake . . . seli zake ndogo katika mwili wake zinajikunja na kupiga mateke na kuruka namna *hiyo*. Lakini anapozaliwa, ana . . . [Ndugu Branham anapiga makofi mara moja, akiiga kipigo—Mh.] namna hiyo, na kisha analia, anakuwa nafsi hai.

137 Na mtoto mchanga anaweza kwenda kanisani na kusema, "Loo, ninaliamini kanisa. Mimi, nitaenda, nitafanya *hivi*. Na mimi ni mzuri . . . Nataka kutenda haki, nataka kutenda haki." Lakini anachohitaji ni pigo la Injili kumwamsha, ili alilie Uzima wa Milele; na Roho Mtakatifu anapiga kelele ndani yake, kama vile Yeye hakuwahi kupiga kelele hapo awali. Halafu ni kiumbe kipya, amezaliwa kwa Roho. Halafu anaanza kukua, kusonga, na kuwa katika Mungu; unaona, kama mtoto mchanga tu, mtoto wa kawaida, alivyo na uhai wake ulimwenguni.

138 Basi kama maskani hii iliyo ya dunia ikiharibiwa, tunayo nyingine inayongojea, unaona. Kwa hakika tu kama vile mwili wa kimaumbile ulikuwa unakuja, kuna mwili wa kiroho kuupokea ulipodondoka kutoka kwa mama yake. Na inapodondoka kutoka kwa mama, ardhi, ambayo ni, uko katika tumbo lake sasa, ukiugua, ukilia, (Ee Mungu!), ukiugua, ukijitahidi, ukizeeka, na ugonjwa, na kila kitu kinachousumbua, na roho iliyo ndani yake ikitafuta nchi ng'ambo ya mto. Inaugua, kupinduka, kuruka, (naam, bwana) kwa sababu kuna maisha ndani ambayo yanaishi milele. Yako katika mwili ambao hauna budi kufa. Na wakati mwingine, kama vile mama alivyodondosha mtoto wa kawaida, na mwili wa kiroho ukampata; dunia itadondoka, na mwili wa kimaumbile utadondoka, na mwili wa kawaida . . . au mwili wa kimbinguni utainyakua kule. Maskani hii iliyo ya kidunia ikiharibiwa, tunayo moja inayongojea. Hiyo ndiyo sababu unasahau mambo ya ulimwengu. Yamekufa, kwako. Huyo hapo Roho.

Sasa iangalie tunapoendelea sasa, hizo roho mbili.

139 Roho Mtakatifu ni Kuzaliwa upya, tunajua hilo. Ni kuzaliwa mara ya pili, na Roho wa Mungu. Hivyo ndivyo unavyozaliwa, na Roho. Kuzaliwa na Roho, hiyo ni Kuzaliwa upya. Vema. Umechukuliwa mimba na Roho; basi wakati unapozaliwa na Roho, unajazwa na Roho Mtakatifu. Vema.

140 Halafu wakati hawa wawili wakiwa duniani, wa kawaida na wa kiroho, wakati mwingine ninii . . . Nimeona hii. Sasa katika kufunga, ninataka kufika mwisho sasa, kwa kusema hili kwa dakika chache. Katika wa kawaida au wa kiroho, mojawapo . . . Sasa natumai kuwa kila mtu anashika hili. Sasa iweni tu watulivu na wenye kicho kadiri mwezavyo.

141 Sasa, mmewahi kuona hii? Unaona katika makanisa yetu leo, hata katika vikundi ambavyo tumejitenga na kuunda madhehebu; na tumeona haya yote. Na ulimwona mtu akichukua Maandiko fulani, na, ndugu, mtu huyo anaweza kuchukua Maandiko hayo na kuyafanya yaishi upya, ayafanye yaishi sawa sawa na yale yaliyoahidi hapa katika Biblia. Na mtu anayefuata atamwona akifanya hivyo, naye atakuja karibu na kujaribu kuifanya, na atashindwa. Natumaini unasoma sasa. Atashindwa. Kwa nini? Maandiko hayajavuviwa kwake. Anajaribu tu kuiga. Anajaribu kuiga kitu fulani. Hakuwa . . . Vema, labda alitumwa na mwanadamu. Labda mtu fulani alisema, "Vema, unaweza kufanya jambo lile lile." Unaona, kama tu vile Yesu alivyosema itakuwa hivi. Biblia inatabiri hilo katika siku za mwisho, "Kama vile Yane na Yambre walivyompinga Musa."

142 Hapo alisimama Musa, na hapo Yambre akasimama. Basi Musa akatupa chini fimbo yake, ikawa nyoka. "Mbona," Farao akasema, "njoo hapa, Yambre, unaweza kufanya jambo lile lile." Na alifanya, unaona. Lakini nini kilitokea? Kisha fimbo ya Musa ikala fimbo yake. Unaona, ilidhihirishwa. Fimbo yake ilikuwa wapi?

143 Kama tu kitu kisichoweza kufikiwa na hisi za kawaida. Ni kama baadhi ya mambo haya ya kimizimu. Ni kama baadhi ya makanisa haya ambayo wanaamini ya kimwili, mbali sana. Mambo ya . . . Wanasema, "Mbona, hiyo ilikuwa kwa ajili ya siku nyingine." Wako nje kabisa. Lakini angalia roho hii katika siku za mwisho inapoenda kuiga Roho halisi. Unaona? Hapo ndipo shida yako inakujia. Sawa kabisa na ile ya kweli, unaona; lakini hakuweza kuidhihirisha, asingeweza kuifanya ishikilie, asingeweza kuifanya idumu. Ee Mungu!

144 Watu huja na kusema, "Nilipata Roho Mtakatifu, pia." Angalia jinsi wanavyoishi; haidumu kutoka uamsho mmoja hadi mwingine, kutoka mkutano mmoja hadi mwingine. Imewekwa wazi, hawajampata. Ikiwa mwanamume amezaliwa kwa Roho wa Mungu, au mwanamke, wana matunda ya Roho. Wanaenenda kitauwa. Wanaishi maisha hayo. Unaona? Wanajiepusha na mambo ya ulimwengu. Mungu hufanya kazi ndani yao na kujidhihirisha Mwenyewe, na kuthibitisha ya kwamba Yeye ni Mungu anayefanya kazi hapo ndani. Mwingine anaiga. Unaona?

145 Uigaji, huo ndio umekuwa kote kote, kuiga. Mwangalie Ishmaeli, na Isaka; na wote kuendelea, unaona, kuiga. Mwangalie nabii Musa, na umwangalie nabii Balaamu. Unaona? Angalia jinsi wanavyoshuka! Mwangalie Yuda, na umwangalie Yesu.

146 Na Yesu anatabiri kwamba huyu Roho Mtakatifu, katika siku za mwisho, atakuwa ndiye Muhuri wa Mungu. Sasa, alama ya mnyama itakuwa nini? Itakuwa ni kukataa Muhuri wa Mungu. Kwa maana, wote ambao hawakuwa na Muhuri wa

Mungu walikuwa na alama ya mnyama. Na ikiwa ni alama mbili za kiroho, moja yao itakuwa alama ya kweli ya Mungu, ile nyingine itakuwa uasi. Je, unaweza kuiona?

147 Angalia alama katika Agano la Kale. Wakati tarumbeta ilipopigwa, yubile, kila baada ya miaka kadhaa, wa—watumwa waliwekwa huru kwa sababu tarumbeta ililia. Vema, kila mtu ambaye alitaka kuwa huru, angeweza kwenda. Lakini wengine wao, walipenda kuwa watumwa, kwa hivyo waliwapeleka kwenye madhabahu na kwenye mwimo wa kanisa, na kutoboa sikio lao kwa uma. Na walitiwa alama milele, walimtumikia bwana huyo wakati wote.

148 Na leo utasikia ujumbe wa Injili juu ya Ukweli, "Sasa unaweza kuwa huru ikiwa unataka," Mungu anasema nawe. Lakini unapofika kwenye mpaka huo hapa na kutazama huko, na kuwa na ujuzi wa Ukweli, halafu ugeuke na kwenda, anakutoboa sikio na daima utakuwa mwaminio wa kiakili. Utakuwa wa kidini na utaenda kanisani, lakini kamwe hutampokea Roho Mtakatifu. Unaona, kisha utumikie hiyo siku yako yote iliyobaki. Sasa, alama ya mnyama, au Muhuri wa Mungu. Na tunakaribia sana.

149 Sasa, angalia, Neno halina budi kuvuviwa; kulisikia, kulitambua, na kuliweka katika matendo. Watu wengi watasikia, lakini hawatalitambua.

Mungu atasema, "Hii ndiyo saa yako."

150 "Nisingekuwa mtakatifu anayejibingirisha. Mimi—mimi sitaki yoyote ya Hilo." Unaona, hawalitambui.

151 Tutaenda kwenye mikutano, Roho Mtakatifu mkuu atashuka. Nilikuwa nimeketi pale siku nyingine, wakati ono lilipotokea na kutabiri kile hasa. Nikasema, "Huyu hapa kijana anakuja." "Njoo hapa," nikamwashiria mhudumu huyo wa hotelini, "una shida ya moyo na unatafuta . . . "

"Ndiyo. Hiyo ni kweli kabisa."

152 "Unamwona yule mwanamke anayekuja pale?" "Njoo hapa. Una uvimbe kwenye titi, na uko kwenye titi la kushoto, na uko katika hali mbaya sana. Na wewe ni mwenye dhambi na usininii . . . "

"Kweli kabisa."

153 Wale watu waliokuwa wameketi pale, walitazama kote, wahubiri na wote, wakasema, "uh-huh!" Nenda kwenye mkutano, angalia Roho Mtakatifu akienda nje kupitia kwenye mkutano na kutaja siri za mioyo, mambo kama hayo. Anasema, "Ajabu. Nadhani. Ndiyo." Unaona? Loo, ndugu! Unaona? Ni—ni—ni upande wa pili, kuna jambo fulani limetokea. Wanawake watazidi kuendelea moja kwa moja, wakifanya jambo lile lile. Wanaume watarudi nyuma moja kwa moja, kama nguruwe

kwenye kugaagaa kwake na mbwa kwenye matapishi yake, vile vile tu. Huoni? Sasa nazungumza na ku-. . . ninii . . .

154 Unaona, lazima utambue basi, rafiki, uko katika hali gani. Hiyo ndiyo sababu kanda hii, nilisema, "Kwa kanisa pekee." Unaona? "Kanisa pekee." Ikiwa umeitwa kutoka kwenye nuru . . . kutoka gizani hadi kwenye Nuru, kutoka mautini hadi Uzimani; kutoka kwa dhana ya kawaida, ya kiakili juu ya Kristo, hadi kwenye ujuzi wa kuzaliwa mara ya pili; na kuangalia maisha yako, kwamba inaweka vitu vya ulimwengu kando, na unamtetea Kristo, haidhuru; basi kuna jambo limetokea. Unaona? Kuna kitu ndani yako, chenye njaa na kinachosonga, kama ilivyokuwa Yakobo. Tazama, unashindana na Bwana, unatembea tofauti baada ya hapo. Kitu fulani ni tofauti ndani yako, umebadilika.

155 Sasa, ndivyo ilivyo, kabla ya kufanywa, lazima iwe imevuviwa kwako. Sijali, ningeweza kusimama hapa na kuhubiri mpaka nipate . . . nywele nilizobaki nazo zianguke, mpaka mabega yangu yainame na niwe na umri wa miaka tisini, na wewe ulisikiliza kila siku; mpaka Mungu akuhuishie hilo, bado uko katika hali ile ile.

156 Siku mbili nimekuwa nikisoma na kuomba juu ya hili. Unaona? Nilisema, "Bwana, niseme hilo kwa kanisa?"

157 Kitu fulani kikasema, "Liseme. Saa imekaribia. Liseme." Ninahisi atakuwa ananivuta kuniondoa hivi karibuni sana, kwa hivyo na—nataka ujue.

158 "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu," alisema Yesu, "isipokuwa Baba Yangu amvute kwanza. Loo, najua mnasema mna Mungu na Ibrahimu, baba yenu; lakini nawaambia hivi, nyinyi ndio . . . baba yenu ibilisi," alisema Yesu. Watu wa kidini, makuhani, na watu mashuhuri, "Nyinyi ni wa ibilisi, baba yenu." Unaona? Angalia, matunda ya Roho.

159 Sasa, unaona, haina budi kuhuishwa kwako.

160 Nisingeweza kumwazia Nuhu akisema, "Unajua nini? Lazima iwe tu huenda ikanyesha siku moja, kwa hivyo nitaenda tu na kujenga safina. Ikinyesha, vema, nitaingia ndani ya safina na kusonga mara moja. Na hakuna kitu kitakachonisumbua, kwa sababu nitaingia ndani ya safina na kuondoka." Je, ungeweza kuwazia? Hapana. Hapana. Hiyo haikuwa hivyo. Ikiwa hiyo ingekuwa hivyo . . . Loo, naomba Wateule waisikie sasa. Ikiwa ingekuwa hivyo, mwenye kudhihaki wa kwanza aliyekuja, kama vile Biblia ilivyosema alikuwapo, alimdhihaki, angeweka nyundo yake chini na kwenda zake.

161 Kama watu wafanyavyo leo hii, wanaoanza na Yesu; na wanapoangalia juu na kuiona Kweli, wanajiepusha Nayo. Hawawezi kuistahimili.

162 Kama yule mwinjilisti maarufu alivyosema, “Ita—itairarua huduma yangu.” Sijali huduma ambayo Roho Mtakatifu angerarua. Inapaswa kuraruliwa. Sasa, lakini, unaona, ni kiburi, ubinadamu mwingi, uanadamu mwingi kupita kiasi. Loo, angalia katika hii sasa.

163 Nuhu alikuwa nje kondeni, akasikia, naye akatambua, na akaweka katika matendo. Haijalishi ni wenye kudhihaki wangapi waliokuja, aliendelea kujenga moja kwa moja.

“Nuhu, wewe ni mtakatifu anayejibingirisha.”

164 “Hainisumbui hata kidogo.” Akaendelea kujenga! Alikuwa amesikia. Alikuwa ametambua kuwa ni Mungu, aliichunguza kwa Maandiko, na ilikuwa hivyo. Aliendelea moja kwa moja kujenga safina, bila kujali.

165 Je, ungeweza kuwazia, ungeweza kuwazia hili, kwamba Musa, akiwa njiani kwenda Misri, alitoka siku moja na kumwambia Sipora, mkewe, “Sipora, unajua nini? Nilipiga msasa kidogo sarufi yangu. Nimenyosha kabisa maskini hisabati yangu, na jiometri yangu na, loo, vitu vingine vingi, na elimu yangu. Kwa kuwa nimekuwa nikichunga kondoo nyuma hapa, ni—ni—nimepiga msasa baadhi ya hizo. Nilifanya kosa kule Misri. Nadhani nitashuka na kulisahihisha. Nafikiri nitashuka”? Hapana, wimbi la kwanza kuja dhidi yake, angeanguka hapo hapo.

166 Alifanya nini? Alisahau yote aliyowahi kujua kuhusu jiometri na juu ya akili yake. Ndiyo iliyomwingiza matatani.

167 Hiyo ndiyo iliyoingiza kanisa matatani leo, ni wahubiri wengi wenye elimu bila kuzaliwa na Roho. Wanaume na wanawake wanapenda kusikiliza hotuba za kiakili, badala ya kuhubiri nguvu na ufufuo wa Yesu Kristo. Hiyo ndiyo iliyotuingiza katika shida leo. Hatuhitaji tena shule za upili na elimu kwa wahubiri. Tunahitaji watu walioitwa na Mungu ambao wamejazwa na Roho Mtakatifu, na sio theolojia ya kujibunia ya dhehebu fulani. Tunahitaji watu walioitwa na Mungu.

168 Musa alikuwa akichunga kondoo, alitulia na kusahau. Alijua akili zake zilikuwa zimeshindwa. Alijua elimu yake ilimpungukia. Alikuwa akichunga kondoo, lakini akasikia, loo, “Vua viatu vyako, Musa, mahali unaposimama ni patakatifu.” Aliisikiliza. Ilikuwa ni nini? Sauti ambayo Malaika alikuwa amezungumza ilikuwa ya Kimaandiko. Alikuwa amemwahidi Ibrahimu, baba yake, “Nitawatembelea watu baada ya kuwa wamekuwa hapa chini kwa miaka mia nne, na nitawatoa kwa mkono wenye nguvu.” Alitambua kuwa hayo yalikuwa ni Maandiko ya Mungu yakidhihirishwa.

169 Hebu nisimame kidogo. Ruhusu hii iingie. Je, mnaweza kuona ninachozungumzia leo? Neno la Mungu linadhihirishwa

moja kwa moja mbele zenu, wala hamtambui. Wazia sasa Sodoma na Gomora; wazia ahadi ya Kristo kwa siku za mwisho.

170 Musa aliitambua; ilikuwa ya Kimaandiko, ilikuwa ni ahadi. Alisikia, akatambua. Kitu fulani kilimwingia, ndugu, angeweza kwenda kuifanya wakati huo. Alitenda. Angeweza kwenda chini na kumzuia kila Farao. Angeweza kuita mapigo wakati alipotaka. Angeweza kufungua Bahari ya Shamu, kwa sababu alikuwa amesikia, alikuwa ametambua, alikuwa akifanya badala ya Mungu.

"Nitakuwa Mungu kwako, wewe uwe nabii Kwangu," Alisema.

Akasema, "Siwezi kuifanya."

171 Akasema, "Vema, basi, wewe uwe mungu, na uache Haruni awe nabii wako. Lazima uende, hata hivyo."

172 Hakusema tu, "Vema, labda ninapaswa kwenda chini na kunyoosha mambo."

173 Ungeweza kuwazia Eliya juu ya Mlima Karmeli, akasema, "Unajua, nchi hii imejaa dhambi sana, labda, labda ninapaswa kutoka na kumwambia Ahabu anapaswa ajionee haya. Labda ninapaswa kwenda juu mlimani pale na kuketi, na kufunga tu muda mrefu, hata watu hao waudhike sana na kuchoka kuniona kule juu nikifa kwa njaa"? Hapana. Hapana. Hiyo haikuwa hivyo.

174 Lakini akasikia, akatambua, akatenda. "Nimewaamuru kunguru wakulishe. Panda huko, karibu na Kerithi."

175 Wakati ulipofika wa maonyesho ya kuamua kati ya Baalim na Mungu, alisema, "Nendeni, mchukue dhabihu zenu, mzifanyie chochote mnachotaka, na mwombe mungu wenu." Wakati walipojikata, na walikuwa na nyama nyingi, na wakaruka juu-na-chini, walikuwa na kelele nyingi, alisema, "Piga kelele zaidi kidogo, labda ameenda, akifuata mahali fulani. Anaweza kuwa amelala." Loo, ndugu!

176 "Vema, unajua nini?" Alisema, "Mimi ni mwaminio wa Yehova, kwa hivyo naweza kufanya hivi, hata hivyo." Loo, hapana, usiige hiyo. Hapana. Usijaribu kuwa Eliya mpaka Mungu akuite uwe. Naam, bwana. "Mimi ni mtumishi wa Yehova." Kuna mia saba wa hao kule chini, pia, lakini hakuna hata mmoja wao aliyethubutu kuifanya.

177 Kisha wakati alipokuwa amekata yule fahali na kumwaga maji, alisema, "Bwana, nimefanya hivi kwa amri yako." Angalia. . .Mtu yeyote mwingine angejaribu, ingekuwa ni kushindwa kabisa.

178 Lazima ivuviwe kwako! Roho Mtakatifu hana budi kuileta na kuidhihirisha kwako.

179 Hiyo ndiyo shida siku hizi. Huwezi kupanda juu, madhababuni, na kusema, "Vema, Haleluya, Haleluya. Bwana, ninataka Roho Mtakatifu. Haleluya, Haleluya." Hapana.

180 Lakini, ndugu, dada, wakati Roho Mtakatifu amelivuvia Neno hilo kwako, utampata kabla ya kuondoka kwenye kiti chako. Kitu ndani yako kimeungua. Mhubiri hatalazimika kukuambia fanya *hivi* na fanya *vile*. Majani ya zamani yataanguka tu, na majani mapya yatakuja. Imevuviwa kwako. Hutamkasirikia mhubiri wakati anahubiri Ukweli kutoka kwenye Biblia. Utaipenda, uiendee. Ni Chakula kwa nafsi yako.

181 Hata Yesu, Mwenyewe, alisema, "Sifanyi kile ninachotaka kufanya, Mwenyewe. Mwana hawezi kufanya chochote isipokuwa kile anachomwona Baba akifanya." Maneno... Alikuwa Imanueli, Mwenyewe. Alikuwa Mungu duniani; Yesu alikuwa. Alikuwa mwili ambao Mungu aliishi ndani. Alikuwa hema ambalo Mungu aliishi chini yake. Amina. Lakini katika hayo yote, Mwana wa Mungu aliyezaliwa na bikira, Imanueli katika utimilifu wa Roho, Yeye alikuwa na Roho bila kipimo. Na, hata hivyo, katika mwili Wake Mwenyewe, alisema, "Sifanyi chochote mpaka Baba anionyeshe kwanza." Ilivuviwa Kwake, kuifanya!

182 Shetani alisema, "Geuza mawe haya kuwa mkate, na ufanye muujiza. Hebu nikuone ukifanya hivyo."

183 Akasema, "Imeandikwa, 'Mtu hataishi kwa mkate pekee.'" Loo, jamani! Lakini wakati umati ulipokuwa na njaa, Yeye alichukua biskuti tano na samaki wawili wadogo, na kuwalisha watu elfu tano. Loo, Haleluya! Unaona ninachomaanisha?

184 Usijaribu kuiga. Hiyo ndiyo shida ya Pentekoste leo. Hiyo ndiyo shida ya kanisa leo, kuna wengi sana wanaojaribu kuiga kuwa wana Roho Mtakatifu. Kuna wengi mno wanaojaribu kuiga uponyaji wa Kiungu. Kuna wengi mno wanaojaribu kuiga mambo tofauti ya Bwana. Huwezi kufanya hivyo. Kwamba mambo huja kwa uchaguzi, Mungu akiita, umeshushwa kutoka tumbo la mama na hiyo. "Karama na miito havina majuto." Loo, jamani! Hiyo ni kweli. Huwezi kujifanya kitu usicho.

185 Lakini ikiwa Mungu anakuita, uwe mtu mwenye shukrani zaidi ulimwenguni kwa sababu amekuita. Basi inakuwa halisi kwako.

186 Kama vile ningeongea, kama ningekuwa na wakati, juu ya kuchakulo siku ile, karibu initie wazimu. Sikuwahi kuiona hapo awali, na sikuweza kuifanya. Hattie, ameketi kule nyuma akiniangalia. Hiyo ingewezekanaje? Haingeweza kuifanya, lakini ilivuviwa, ikahuishwa. Neno lilinenwa na likafanywa hivyo. Haleluya!

187 Paulo, ungeweza kumwazia akisema, "Nimekuwa nje kwenye bahari hii kwa siku kumi na nne mchana na usiku, na hakuna nyota wala mwezi, au jua au chochote. Nadhani

nitaenda tu huko na kuwaambia, 'Jipeni moyo, maana Mungu atatushughulikia, kwa vyovyote vile'"? Loo, Mungu hafanyi kazi namna hiyo. Mungu hafanyi hivyo.

188 Imani yako ni sawa, ndugu. Imani yako ni ya ajabu. Lakini mpaka jambo hilo limevuviwa kwako!

189 Loo, hii hapa taa nyekundu imening'inia hapo, na ikiwa nitaona. . . Nasema, "Vema, nimeweka mguu wangu kwenye kichapuzi. Nina gari. Ninaweza kupitia hiyo nuru kule, nikienda maili mia na ishirini kwa saa." Hiyo ni kweli. "Ninaweza kuhisi nguvu chini ya mguu wangu." Lakini ni afadhali usubiri mpaka ishara ya "nenda". Haleluya!

190 Je, mnaelewa kile ninachomaanisha? [Kusanyiko Linajibu, "Amina."—Mh.] Wakati ishara ya "nenda" ikija, sawa. Wakati jambo hilo limevuviwa kwako, na Mungu analifanya lifahamike kama alivyofanya huko nyuma, sawa. Lakini mpaka atakapofanya hivyo, tuna kundi la watu wa Yuda wanaoiga, wakitembea kama, tuseme, "Naam, mimi ni sawa tu na wao. Mimi ni Mkristo, pia."

191 Loo, hukumbuki? Wana wa Skewa—Skewa, walitoka nje wakasema, "Tunakuapisha, tunakuapisha kwa Jina la Yesu ambaye Paulo anahubiri. Toka!"

Akasema, "Paulo namjua, na Yesu namjua, lakini wewe ni nani?"

192 Saa inakuja wakati haki na batili vimedhihirishwa. Inaonyesha katika Wakristo leo. Inaonyesha katika makanisa leo. Inaonyesha katika watu leo hii. Ninawaweka kwa muda mrefu; nataka hii iwafikie.

193 Paulo hakusema, "Ninaamini nitapanda tu juu na kusema, 'Vema, kuwa na ujasiri mwingi.'" Hapana.

194 Alifanya nini? Alisikia Malaika. Alijua kwamba huyo alikuwa ni Malaika yule yule ambaye alikuwa akiongea naye kila wakati. Alitambua, kisha akatenda. Akainuka na kusema, "Kuwa na ujasiri mwingi. Kwa maana Malaika wa Bwana, ambaye mimi ni mtumishi Wake, alisimama karibu nami jana usiku, akinionyesha ono kwamba hakuna chochote kitakachopotea, kwenye meli hii. Kuwa na ujasiri mwingi. Nenda ukale chakula chako cha jioni sasa. Kila kitu ni shwari." Amina. Wakati imevuviwa kwako, wakati Mungu anaifanya sawa!

195 Nilipata maoni hapa mahali fulani, nilikuwa nimeandika. Haya hapa papa hapa. Uh-huh. Tuko mwisho wa mambo yote. Acha nilete hii namna hii sasa, katika kufunga. Natumaini kuwa Mungu amekufunulia jambo. Angalia. Kila kitu kiko mwisho. Mtu fulani aliuliza hivi majuzi usiku, naamini ilikuwa ni Ndugu Fred Sothmann, tulikuwa tunauliza kuhusu jinsi wakati wa mwisho umekaribia.

196 Ndugu Demos Shakarian alikuwa ameona ono hilo likidhihirishwa sana, na likatimia siku tano baadaye, kikamilifu, karibu limwondoe kwenye viatu vyake. Aliniita. Akasema, "Joseph yu hali gani?"

Nikasema, "Mzima."

Akasema, "Yeye huona maono?"

197 Nikasema, "Naam. Aliniambia kuhusu David, mtoto wa Ndugu Wood, ambapo alikuwa ameanguka kwenye pikipiki, siku tatu au nne kabla halijatokea, hasa kabisa."

Akasema, "Unajua, vitu hivyo hufuata familia."

198 Nikasema, "Haki au uovu, hufuata, mojawapo. Inafuata familia."

199 Na tulikuwa tukiongea kidogo, na wao, Fred akaniambia, "Hii imetolewa wapi, Ndugu Branham?"

200 Nikasema, "Angalia, Fred, hebu tuichukue kwa maumbile. Mungu hufanya kazi katika maumbile yake. Angalia, angalia kilichotokea. Jua lilichomoza Mashariki. Huo ndio ustaarabu wa kale kuliko wote tulio nao, ni Uchina." Sisi sote tunajua hilo.

201 Ustaarabu wa kale kuliko wote tulio nao ni Uchina. Vema. Na ustaarabu umeelekea upande wa magharibi wakati wote. Na sasa ungeondoka wapi ikiwa ungeondoka Pwani ya Magharibi, ukivuka moja kwa moja? Unaenda Uchina. Hasa. Tuko mwisho. Biblia ilisema, nabii alisema, "Kutakuwa na siku ambayo haitakuwa usiku wala mchana, wakati jua linapita, lakini wakati wa jioni," kabla tu ya kuishia hapa, "tena itakuwa Nuru, vivyo hivyo." Yesu alisema, "Kutakuwa na mvua ya masika na mvua ya vuli. Na mvua ya vuli itatoa mvua ya masika na ya vuli pia, katika msimu huo huo." Tuko katika wakati wa mwisho.

202 Angalia hapa, hebu nikuonyeshe. Siasa iko mwisho. Je, mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Nionyeshe kitu leo . . .

Taifa hili ndilo baya kuliko yote duniani, kwa ufisadi, uovu. Nani aliyesoma gazeti la Courier Journal hivi majuzi usiku, huko Louisville, wakati wanawake hawa wote, wakichagua, kila taifa, mwanamke aliye mrembo kuliko wote katika taifa hilo, na kuwasimamisha kuwa Mrembo wa Ulimwengu? Kila mtu alifanya isipokuwa Urusi. Nao wakampelekea Khrushchev na kumwuliza, "Kwa nini isiwe hivyo?" Akasema, "Urusi haiwavui nguo wanawake wao, ili watembee mbele ya wanaume." Taifa la kipagani, kafiri likileta aibu juu yetu sisi tunaojiita Wakristo, akasema, "Urusi haiwavui nguo wanawake wao, ili watembee namna hiyo. Na kamwe huoni kaptura au vitu kama hivyo huko Urusi." Hao ndio wapagani. Na sisi ambao tunajiita "Wakristo"!

203 Si ajabu Biblia ilisema, "Kila meza imejaa matapishi. Na ni nani ninayeweza kumfundisha Mafundisho, na ni nani aliyeachishwa maziwa? Lakini amri itakuja juu ya amri, na

mstari juu ya mstari. Maana kwa midomo ya kigugumizi na kwa lugha zingine nitazungumza na watu hawa. Na hii ndiyo Raha. Kwa haya yote, hawangeweza kusikia." Tulipata dhana yetu wenyewe ya kiakili. Loo, jinsi ingekuwa vizuri kukaa siku nzima juu ya Hilo.

204 Siasa, zimechafuka! Wanademokrasia, Waripablikani, na wote, ni duni sana. Ni kitu gani? Ni kundi la ufisadi. Kila mtu anayefanya kazi ndani yake, ambaye hajazaliwa mara ya pili, ni wa ibilisi. Ibilisi alisema, "Kila ufalme duniani ni wangu," na Yesu kamwe hakubishana naye. Ulimwengu unatawaliwa na ibilisi. Na kila mtu anayefanya kazi kwa serikali, ikiwa si Mkristo, yeye ni wa ibilisi na anamfanyia kazi ibilisi. Mataifa haya yote yatamwangukia Yesu Kristo atakapokuja, kutakuwa na Utawala wa Miaka Elfu.

205 Angalia hapa leo, kile wanachoendea sasa. Kunipigia kelele kuhusu kutumia pesa huko nje kwa ajili ya Wakristo, na kutaka kunipa miaka ishirini katika gereza la serikali, kwa kutumia pesa kutekeleza huduma ya kidini. Na wiski na bia na sigara huondolewa makumi ya mamilioni ya dola kwa mwaka, ili kuharibu taifa. Nami nikijaribu kuhubiri haki, nikisimama katika mlango wa Yesu Kristo, na kunipeleka gerezani kwa sababu yake. Na kuchukua vitu kama hivyo vya waovu, walio duni, werevu, wenye akili, na kuwaacha waiondolee mbali kwa vipindi vya runinga ambavyo viliharibu ulimwengu, vikawafanya wanawake kuwa kama takataka. Moja ya laana kubwa zaidi ambazo taifa limewahi kuwa nazo, na wanapita nayo. Wananipeleka gerezani kwa kuhubiri Injili, nikichukua dola chache hapa kwenda ku—kuhubiri Injili, ambayo watu hunipa nihubirie Injili. Mimi sio tajiri na siwezi kuondoa hiyo. Lakini bado wanataka kunipeleka gerezani, kunishikilia miaka miwili, na nina kesi inayokuja hivi karibuni. Loo, jinsi ilivyo duni, jinsi ilivyo chafu! Mungu, turehemu.

206 Nitasema jambo hili moja, labda hivyo ndivyo Mungu alivyofikia kabla hajatuma bomu la atomiki. Lazima ufanye kitu kibaya, unajua. Huna budi kugusa watiwa-mafuta wake mara moja, kwa Andiko hili hili, isije hiyo . . . "Usiguse Wateule Wangu." Hiyo ni kweli. Kwa hivyo ikiwa inabidi ichukue hiyo kuleta hukumu, kama ilivyofanya katika siku za Danieli au mahali pengine, acha ije. Mimi ni mtumishi Wako, Bwana. Hiyo ni kweli. Loo, naam.

207 Siasa, duni kabisa! Taifa, limeharibiwa! Kweli, angalia nini! Wataweka askari waliovalia kaptura sasa. Loo, jamani! Siasa, vita! Siasa iko mwisho. Watawala wa kimabavu wamekosea. Siasa ni mbaya. Kwa nini hawakukaa na mfalme mtauwa kama Mungu alivyowapa, Daudi? Bwana mkubwa wa Uingereza alisema, wakati hii—wakati demokrasia hii iliundwa, alisema, "Ni sawa sasa hivi, lakini itafika wakati," alisema, "haitakuwa chochote. Itakuwa maneno matupu." Na yeye yuko sahihi.

Akasema, "Wanasiasa husimama juu ya masanduku ya sabuni kwenye kila kona, kila namna ya mambo mapotofu ambayo yanaharibu serikali." Na mtu huyo alikuwa sahihi. Kile hasa kinachoendelea.

208 Mtu mmoja anaweza kwenda hapa nje, na kupita hapa na kulewa, na kurarua kila kitu anachotaka kurarua; na kwenda huko chini, anajua kila mtu, kwa hivyo hakuna chochote kinachosemwa. Hebu mtu maskini, au mtu fulani asiyejua, ajaribu kufanya hivyo, na wanapelekwa gerezani. Ufisadi, duni kabisa, uchafu, asilimia arobaini ya hao ni mashoga. Wazia hilo, Sodoma na Gomora tena! Hilo hapo kundi, linalodhaniwa kuwa la kidini.

209 Na—nashangaa ni nini kinatokea baadaye, wakati Rais ajaye akiingia? Mungu ametupa mtu mmoja mzuri mtauwa, mzee Dwight Eisenhower. Na sasa natu-. . . Angalia ni nini kitu kinachofuata. Na tunaweza kuwa na mhuni wakati ujao, hakika kabisa. Lakini kunakuja, "Farao ambaye hamjui Yusufu." Kumbuka hilo. Nitafikia hilo kwa sekunde moja tu. Siasa zimechafuka. Tunajua hilo.

210 Vita viko kwenye mwisho wake. Loo, walirushiana mawe mmoja kwa mwingine, walipigana kichwani kwa mashoka ya mawe, kisha wakarusha uta na mshale. Halafu wakapata bunduki, kisha bombom, kisha themanini na nane huko Ujerumani, na bunduki kubwa sana na sisi. Kisha wakarusha mabomu ya mkono na gesi ya sumu. Lakini wana bomu la haidrojeni sasa. Vita viko mwisho. Kila taifa linayo, kwa hivyo utafanya nini sasa? Hata taifa dogo leo, kufyatua tu bunduki kiwazimu, hayo ndiyo yote wanayopaswa kufanya, na wote unalipuka. Vita viko mwisho. Huh! Amina. Vita viko mwisho. Siasa ziko mwisho.

211 Elimu iko mwisho. Uhalifu wa vijana uko mwisho. Watoto, hakuna matumaini kwa watoto, wameingia wazimu. Huwezi kuwa na elimu. Huwezi kwenda hapa shuleni na upate, kupata mtoto mwenye elimu. Yeye ni—yeye ni mtoto mara mbili zaidi ya kuzimu wakati anatoka kuliko alivyo wakati akiingia. Hebu mwalimu aseme kitu juu yake, atauawa. Wataunda Klux kidogo na kwenda huko nje na kumpiga risasi mwalimu, kumtoa nje na kumfunga kamba. Tulipoteza walimu elfu mbili. Loo, ngoja kidogo, naamini ilikuwa ni walimu elfu ishirini, mwaka huu uliopita. Siwalaumu. Nisingetaka kuifanya, pia. Sasa walikuwa na ishara kila wakati, "Wape watoto hawa elimu ya vyuo." Wanaihitaji, lakini ibilisi amewapata. Ibilisi amewapata. Na sio kawaida tu kwenda nje na kuwa mbaya na—na—na kuondoa lango na kulitundika juu ya mti kwenye usiku wa Halloween, au ufanye ujinga kidogo kama watoto walivyokuwa wakifanya, au kuchukua mkokoteni wa mkulima na kuuweka barabarani, sio hivyo; lakini wao ni wendawazimu. Wanafanya mambo ambayo

ni wendawazimu; kukupiga risasi, kukuua, kukuua kinyama, kukupa sumu, chochote kile. Hicho ndicho kizazi kinachofuata.

212 Kuzaa watoto kuko mwisho, uwanamke, umama. Kwa nini, udhibiti wa uzazi unafanywa kila mahali, na mbwa wadogo wamechukua mahali hapo.

213 Maadili, hakuna maadili kwake tena. Wanawake, wakivalia vibaya; kuja kupitia runinga, kila namna za uigaji wa watu waovu wa Hollywood, kila namna ya vitu, mitindo. Yote yako mwisho!

214 Elimu iko mwisho. Siasa ziko mwisho. Vita viko mwisho. Ustaarabu uko mwisho. Vitu hivyo vyote viko mwisho. Jamani, tunaweza kufanya nini basi? Ni nini kinachofuata? Tuko mwisho wa mambo yote.

215 Sasa maisha ya kanisa yako mwisho, kanisa la kawaida, kanisa. Sasa, hii inaweza kushikamana kidogo tu, lakini kanisa la kimwili, kanisa la Esau, limefika mwisho wake. Anafanya nini? Kuelekea katika shirikisho la makanisa, ambalo mwishowe litajiunga na Urumi, kupigana na Ukatoliki . . . au na Ukatoliki kupigana na ukomunisti. Papa John anatoa wito kwa makanisa yote kurudi, na watarudi. Na watajiunga pamoja, sawa kabisa na BWANA ASEMA HIVI.

216 Unasema, "Ngoja kidogo, Ndugu Branham. Unaondoka kwenye mstari." Ikiwa niko nje ya mstari, Mungu aliandika Biblia Yake mbali na mstari. Lazima uwe Mikaya, kwenye kisa hiki.

217 Morris Cerullo aliniambia hivi majuzi usiku, akasema, "Yuko wapi mpinga Kristo, Ndugu Branham? Myahudi ndiye mpinga Kristo."

Nikasema, "Morris! Na wewe, Myahudi?"

Akasema, "Hao ndio wachukia-Mungu kuliko wote waliopo."

218 Nikasema, "Morris, usithubutu! Niambie katika Maandiko ambapo mpinga Kristo alitoka Yerusalemu. Mpinga Kristo alitoka Rumi, sio kutoka Palestina."

Akasema, "Vema, angalia, mimi niko . . . Wao ni wachukia-Mungu."

219 "Naam, hivi Mungu hakusema alipofusha macho yao ili tuweze kuwa na siku ya kuona? Lakini siku yetu itakuwa imekwisha hivi karibuni."

220 Akasema, "Loo, Ndugu Branham, sikuwahi kufikiria jambo hilo." Angalia, haya basi.

221 Tazama, tuko mwisho. Ulimwengu wa kimwili, kanisa la kimwili liko hapo, mwisho. Angalia jinsi linavyoelekea katika shirikisho la makanisa. Ndugu wa Umoja waliingia ndani yao. Pentekoste iko ndani yao. Wengine wote wanajiundia dhehebu.

Tuwaone huko chini, hao Wakanaani, kote kote kupitia hizo roho za Esau, za kidini sana, na kujishirikisha na ulimwengu; sio ufahamu wa kiroho, usioweza kushinda, si mteule wa Mungu, kuitwa na kutengwa.

222 Loo, laiti ningeweza tu kuifanya ijulikane, wakati ikiwa ningeweza kuisukuma chini kwa njia fulani! Hawaioni. Wana macho na hawawezi kuona, masikio na hawawezi kusikia. Loo, kwa nini sisi ni wazito sana katika Roho? Sasa, sikiliza hii. Kila kitu kiko mwisho.

223 Na Kanisa la kiroho liko mwisho Wake. Linakuja mwisho. Ee Mungu! Angalia huko nyuma wakati alipoanza na Luther, akatikisa, wa kiroho. Halafu na Wesley, akaja kwenye utakaso. Halafu na Pentekoste, Roho Mtakatifu. Na sasa wakati wa mwisho, Roho wa Kristo katika Kanisa, anafanya kazi zile zile alizofanya, kurudi kwenye Kichwa Chake tena; tayari kwa Kanisa na Kristo kuungana, na Kuja kwa Bwana Yesu, na ufufuo wa wafu. Tuko katika wakati wa mwisho. Yesu alisema hivyo, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu." Je, unaelewa hilo?

224 Angalia kanisa la kimwili. Angalia mahali wanakoelekea, mbali zaidi na mbali zaidi.

225 Angalia Kanisa lililojazwa na Roho, ukitikisa na kuondoa maskini upuuzi wake wote, akipanda katika Roho, (kwa uchache, bila shaka), akija katika Roho, lakini tukisogea mahali kama hapo mpaka imefika mahali ambapo Roho Mtakatifu anatembea kupitia Hapo, akifanya njia Yake, tayari kumpokea Bwana wake, tayari kumpokea Bwana wake.

226 Na hao wengine wote walijiundia dhehebu, wakirudi ulimwenguni, wamejitenga, wakirudi katika shirikisho, wakiingia kwenye kichwa hicho kimoja kikubwa shirikishi chini ya Ukatoliki. "Na sanamu ilifanyizwa kwa huyo mnyama." *Sanamu,* "kitu kinachofanana naye." Shirikisho la kanisa lililoundwa na Ukatoliki, hao wawili pamoja, hufanya kazi pamoja. "Ni nani anayeweza kupigana na mnyama au sanamu yake?" Kwa kweli sivyo. Jinsi tungeweza kuipitia kwa saa kadhaa!

227 Sasa hebu niwaambieni hili, na kisha itakuwa ni wakati wa kufunga. Ni mimi nimeninii. . .Niliwaambia ulikuwa unaenda kuwa mrefu. Ni—ninajihisi tu kuwa nimefungwa. Wakati Mungu hata alisema mambo haya, akasema, "Waambie. Lizungumze. Usinyamaze tena. Waonyeshe. Wasipolipokea, basi damu haiko mikononi mwako." Saa imewadia. Wakati, yote yanapanda juu.

228 Ulimwengu uko katika mwisho wake. Hauwezi kusimama zaidi. Vita viko mwisho wake. Huwezi kuwa na vita tena. Ikiwa una vita, haitakuwa; kwanza tu anafyatua bunduki, ndivyo ilivyo. Siasa, imeoza na kuchafuka.

229 Ulimwengu wa kanisa ni Wamethodisti, Wabaptisti, Wapresbiteri, Wapentekoste. "Ni nguruwe kwenye kugaagaa kwake, mbwa kwa matapiko yake." Hiyo ni kweli, kila mmoja wao! Mungu anaita, kutoka kwa ufisadi huo, Kanisa lililochaguliwa. Hiyo ni sawa kabisa. Esau, wakasema, "Sisi ndio kanisa!" Sina shaka na hilo. Yakobo alikuwa baba wa Esau, pia, hiyo ni kweli, hivyo, lakini—lakini . . . Namaanisha, Isaka alikuwa baba wa Esau, na Yakobo alikuwa nduguye, pamoja naye. Lakini mmoja alikuwa na malipo kwa haki ya mzaliwa wa kwanza; yule mwingine aliichukia. Mmoja alisikia, akatambua, na akaweka katika matendo. Yule mwingine akasema, "Loo, maadamu ninaenda kanisani na kufanya yaliyo mema, inaleta tofauti gani?" Wewe hapo. Sasa ndani . . .

230 Ninasema hivi basi, katika kufunga, tamshi hili moja zaidi. Kanisa halisi lina mengi ya kuishia sasa. Loo, inapaswa kuwa wakati wa kufurahia sana kwa Kanisa la kweli, kwa Kanisa la kweli, kwa Kanisa teule, wakati unajua moyoni mwako umepita kutoka mautini kuingia Uzima; unapojitazama mwenyewe na kuona, kuangalia maisha yako na kuona kuwa vitu vyote vya ulimwengu vimepita, kwamba umekuwa kiumbe kipya. Sikiza sasa, katika kufunga, kwa makini. Unajua kwamba umepita, maisha yako yanaithibitisha, "Kwa matunda yao mtawatambua." Lengo lako lote ni Kristo. Unamtarajia Yeye kuja wakati wowote. Unatembea katika Roho. Unampenda. Unamwona akifanya kazi kupitia wewe. Hakuna kitu ambacho unatamani kufanya, lakini Yeye huifanya tu, Mwenyewe. Loo, ni wakati wa jinsi gani!

231 Inanikumbusha juu ya mwanasanaa ambaye alikwenda Roma, kujifunza kuwa mwanasanaa, jamaa mdogo. Walimwona. Alikuwa tofauti sana na wavulana na wasichana wengine wote wa Marekani, na kadhalika ambao walienda huko kuwa wanasanaa, na kutoka kwa ulimwengu wote. Kijana huyu mmoja alikuwa bora. Alikuwa mtu mzuri, na walitambua. Wangekuwa na sherehe kubwa, na kufika huko na, jinsi wanavyofanya huko Roma, kulewa tu kwa kadri wanavyoweza.

232 Nimekuwa huko, mwenyewe, na kuwaona. Wanatoka nje barabarani, wanaume na wanawake, na kufanya yasiyofaa. Hata katika mabustani, wanafanya mambo ya ngono ndani ya bustani, moja kwa moja hadharani, bila kujali; Uingereza, pia, wengine wote. Unaona? Hiyo si mbaya zaidi kuliko hapa. Jambo lile lile tu hapa, mbaya tu karibu hivyo; ila tu, wanaifunika tu zaidi kidogo hapa, kwa mujibu wa polisi na kadhalika. Sasa, lakini ni mbaya kabisa!

233 Vema, kijana huyu, alijiweka mbali na hayo yote. Wakati wanaenda kwenye karamu zao, angewaacha waende, lakini alikuwa anajifunza kuwa mwanasanaa. Kwa hivyo, siku moja maskini msimamizi, ambaye alikuwa Mkristo ambaye alikuwa karibu na ju—jumba la makumbusho, nyumba ya sanaa,

alisema—alisema, “Hebu tutembee kidogo, mwanangu. Hebu tutembee, ningependa kuzungumza nawe kidogo.”

Akasema, “Sawa.”

234 Kwa hivyo walienda, wakikwea kilima, na wote wawili mikono yao nyuma yao, walikwea kilima. Jua lilikuwa likizama. Na kwa hivyo yule mzee akamwambia msanii mchanga, akasema, “Mwanangu, wewe ni Mmarekani.”

Akasema, “Ndiyo.”

235 Akasema, “Ulikuja hapa kupata elimu yako katika sanaa. Nadhani una lengo la kufanya kazi ya maisha yako kama mwanasanaa.”

Akasema, “Ninapanga kufanya hivyo, bwana.”

Akasema, “Ninaona kuwa wewe ni Mkristo.”

Alisema, “Mimi ni Mkristo.”

236 Akasema, “Kweli, kuna jambo moja ningependa kukuuliza. Nimewauliza hawa wengine. Wanasema wao ni Wakristo, pia.” Akasema, “Ni nini kinachokufanya uwe tofauti sana? Ni nini kinachokufanya uwe tofauti na hawa wavulana wengine kutoka Marekani, na wasichana hawa kutoka Marekani? Ni nini kinachokufanya kuwa tofauti sana, na hata hivyo nyote mnasema nyinyi ni ‘Mkristo’?”

Akasema, “Bwana, unaona vile jua linazama?”

Akasema, “Ninaona.”

237 Akasema, “Huko ng’ambo ya bahari, katika jimbo fulani huko New England, katika jiji fulani katika jimbo hilo, na katika nyumba fulani katika jiji hilo, kuna msichana fulani ambaye niliahidi kwamba nitaishi mwaminifu kwake.” Akasema, “Hiyo yote iko kwenye mawazo yangu, kupata elimu yangu ya sanaa na kurudi kwa msichana huyo ambaye anaishi mwaminifu kwangu.” Akasema, “Ndivyo ninavyoishi vile ninaishi.”

238 Loo, ndugu, dada, unaweza kushangaa kwa nini hatujali kile wanatuita. Sijali wanachosema.

239 Nilikuwa nimesimama na Fred hivi majuzi, kule San Juan, Puerto Rico, nilikuwa nikitazama ng’ambo ya bahari, na nikaona huko, ule mwamba wa matumbawe, nusu maili nje, mawimbi hayo makubwa yakipasuka. Akasema . . . Flamingo wanaotembea kwenye bustani, na kadhalika. Nikasema . . . Akasema, “Ndugu Branham, hii ni kama Mbingu.”

240 Nikasema, “Lakini bahari itatulia huko, ndugu.” Nikasema, “Ng’ambo ya bahari tu kule, kuna mahali fulani panapoitwa Mbingu, kuna Mtu anayeitwa Yesu, katika Mbingu hii, kwamba siku moja aliondolea mbali dhambi zangu zote. Nami nilimwahidi nitaishi mwaminifu Kwake, nitafanya mambo ambayo alitaka nifanye. Hiyo ndiyo sababu sioni aibu kwa Injili yake, Hiyo ni Nguvu za Mungu kwa wokovu.” Hiyo ndiyo

inayomfanya Mkristo kuishi tofauti. Yeye ni tofauti kwa sababu ana Kitu cha kuishia tofauti.

Hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja.

241 Rafiki yangu aliyefadhaika, asubuhi ya leo, una kitu tofauti cha kuishia, kitu cha kukutoa ulimwenguni, kitu ambacho kina maana zaidi kwako kuliko ulimwengu wote, ni kumwishia Kristo? Ikiwa hujapata hicho, kwa nini usikipokee sasa. Usiende tu kanisani na kusema, "Nataka kuwa mtu mzuri." Usifanye hivyo. Unataka kuwa Mkristo. Wewe, ikiwa kuna jambo ambalo limekuwa moyoni mwako kila wakati, likikwambia, "Huko sawa, lakini nataka uwe sahihi." Umekuwa ukitamani sana kuwa kitu usicho sasa, hujui kwamba hilo ni Mungu akikuita? Usiligeuzie mgongo wako. "Kwa maana ikiwa uliwahi kuangaziwa na ukapata fursa, na ukaikataa mara yako ya mwisho, hakubaki dhabihu tena kwa ajili ya dhambi." Usiambatane na Esau.

242 Njoo na Yakobo, bila kujali . . . bila kujali kitakachokugharimu. Ikikugharimu nyumba yako, ikikugharimu kazi yako, ikigharimu mume wako, ikigharimu mke wako, ikigharimu watoto wako, ikigharimu chochote, pata haki hiyo ya mzaliwa wa kwanza! Hiyo ndiyo muhimu. Na ikiwa unajisikia hivyo juu yake, asubuhi ya leo, na ungependa kupata haki hii ya mzaliwa wa kwanza! Siwezi kukupa Hiyo. Mungu anaweza, na Yeye Ndiye anayezungumza nawe. Waweza kuinua tu mkono wako, useme, "Niombee, Ndugu Branham. Haki hiyo ya mzaliwa wa kwanza, ninaitaka." Mungu awabariki, kila mahali kote. "Haki hiyo ya mzaliwa wa kwanza, ninaitaka."

243 Baba yetu wa Mbinguni, ninakushukuru Wewe, Mungu Mtukufu Sana na Mtakatifu, kwa wema Wako wote na rehema kwa wana na binti za wanadamu. Na tunatambua kuwa tuko katika wakati wa mwisho, hakuna kitu kinachoweza kuendelea zaidi. Tunasubiri tu kwa wakati wa kuazima; kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, uvumilivu wa Mungu, wakati safina ilikuwa ikiandaliwa, wakati watu wanane tu waliokolewa. Ulisema, "Ndivyo itakavyokuwa wakati wa kuja kwake Mwana wa Adamu. Uvumilivu wa Mungu, hataki kwamba yeyote aangamie, lakini ili wote wafikie toba."

244 Na leo katika jengo hili, kuna wanaume na wanawake wameinua mikono yao, wavulana na wasichana, vijana kwa wazee, wameinua mikono yao, na kusema, "Kuna Kitu kinanivuta." Ee Mungu, naomba wasiikatae Hiyo. Naomba wauze elimu yao, na wauze kila kitu walicho nacho. Kama yule mtu aliyepata lulu kubwa; ilikuwa lulu mashuhuri, kubwa, ilikuwa lulu kubwa kabisa, na akauza watoto wake wote, ili anunue lulu hii kubwa, mashuhuri. Na wauze kila kitu walicho nacho cha ulimwengu, asubuhi ya leo, umaarufu wao wote wa ulimwenguni.

245 Hawa wanawake walioketi hapa, Bwana, wengi wao ambao wamesikia Injili ikihubiriwa mara nyingi sana, na bado wanaendelea kuingia moja kwa moja ulimwenguni, na mitindo kama ulimwengu na kuvaa kama ulimwengu, na kwenda kwenye tafrija na vitu ambavyo ulimwengu, wakishiriki vitu vya kidunia na kutenda kama ulimwengu, na kutumia vitu vya ulimwengu. Ee Mungu, hebu waaibike, asubuhi ya leo. Ikiwa kuna matumaini yoyote ndani yao, Bwana, yageuze leo. Hebu hii iwe ndiyo saa.

246 Na watu hawa hapa, Bwana, Ee Mungu, warehemu. Wengi wao bado wanatembea katika vitu vya ulimwengu, bado wanatamani na kufurahia mambo ya ulimwengu, dhambi, kuvuta sigara, kunywa pombe, vileo, bia kidogo pembeni, au—au kitu kama hicho, au wangekuwa na tamaa mbaya, na kutundika picha ukutani, wasichana waliovalia kizinifu. Na hiyo miili ambayo wanaiangalia barabarani, na karibu wanakanyaga watu kuwatazama, wakijiita wenyewe Wakristo.

Na ujue kwamba umbo hilo la mwili wa mwanamke huyo, labda katika masaa ishirini na nne, litakuwa likiozea huko kaburini, wadudu na mabuu wakitambaa kupitia viungo hivyo vilivyoumbika vya mwili wake; na nafsi yake kule kuzimuni kwa ibilisi, kwa jinsi alivyoishi. Na, hata hivyo, angeweka midomo yake midogo, iliyopakwa rangi, na kubeza na kukucheka.

247 Mungu, warehemu watu hao. Ee Bwana, usiwaache wapotee. Naomba uwarehemu na utume rehema. Mpe kila mmoja wao, Bwana. Wewe Ndiwe pekee unayeweza kutoa baraka hii. Na ikiwa umewaita kwenye Uzima wa Milele, jalia mioyo yao ifunguke; na waweke kila kitu kando asubuhi ya leo, halafu wataipokea. Ijalie, Baba.

248 Na sasa Roho Mtakatifu na aje kwenye mkutano huu, kwa ajili ya wagonjwa na wanaoteseka, pia jalia watu waone kwamba Ujumbe huu ambao umehubiriwa asubuhi ya leo, kwamba Kuja na kila kitu kuko mwisho, na hata Yesu anafanya kazi katika Kanisa Lake. Jalia itimie sasa hivi, Bwana, kwamba Wewe unaweza kuwachukua watu hawa mikononi Mwako. Na wanapoona Roho Mtakatifu akifanya kazi, akitembea kati ya watu, naomba ithibitike, Ujumbe ambao nimehubiri, kwamba tuko katika wakati wa mwisho. Na hebu wasikie. Wamesikia, na hebu watambue ya kwamba Yesu yuyo huyo, jinsi alivyofanya katika siku Zake, Yeye yupo hapa akifanya kupitia Kanisa Lake katika siku ya mwisho. Na basi hebu watende, kwa kutoa maisha na miili yao, na nafsi na roho, Kwake. Ninawakabidhi Kwako, Bwana, katika Jina la Yesu.

249 Sasa, katika jengo ambalo watu wako, nilimtuma Billy asubuhi ya leo kutoa kadi za maombi. Yeye. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

250 Je, wewe ni mgonjwa, mhitaji? Ikiwa Mungu atanifunulia, kama vile alivyomfanyia yule mwanamke kisimani, na kuniambia shida yako ni nini, au jambo fulani kukuhusu, ambalo unajua kwamba sijui, ingekufanya uwe na imani ya kumwamini Mungu? Je, itawafanya ninyi wengine kuwa na imani? Je, hii ndiyo mara yetu ya kwanza kukutana? [Dada huyo anasema, "Hapana"—Mh.] Loo, uliniona hapo awali, lakini mimi ni mgeni kwako. Hiyo ni kweli? Vema, Bwana Mungu akupe haja yako.

251 Sasa, ni halisi, au sivyo? Loo, jamani! Iteni dini yenu ya kiakili. "Baalim," akasema, "yuko wapi?" Eliya juu ya Mlima Karmeli, alisema, "Baalim yuko wapi? Wapi? Mwamsheni." Haikubidi kumwamsha Yesu. Yu macho wakati wote. Yeye yupo daima, yu hai wakati wote, ana uwezo wakati wote; yeye yule jana, leo, na hata milele. Amina. Mungu anabaki Mungu.

252 Unaamini shida yako ya moyo itakuacha na utapata afya? Hutoki hapa. Wewe rudi Lexington na uwaambie watu ni mambo gani mazuri ambayo Bwana amekufanyia. Unaona?

253 Inapita juu ya vichwa vya watu, ambao hawaipati. Kanisa hai lingeshika hiyo, upesi, na kujua kwamba Uwepo wa Roho Mtakatifu upo hapa.

254 Mtu fulani hapa ndani aliinua mkono wake. Ilikuwa wewe, mama? Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yako? Maskini . . .

255 Ndugu huko nje mwishoni, naamini alisema, muda mfupi uliopita, hiyo. Unaamini, ndugu? [Ndugu huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Unaamini? Basi shida hiyo ya ngozi itakuacha, utakuwa sawa. Je, unaamini huo? Je, unaukubali kuwa ni kuponywa? Inua mkono wako, kama unaamini. Unaona? Uh-huh. Vema. Yeye ni mgeni kwangu. Unajua hilo, Pat.

256 Mwanamke anayeangalia pale, akiomba, alinitazama, akasema alikuwa mgeni. Unaamini shinikizo hilo kuu la damu litakuacha? Hiyo ni kweli, sivyo? Inua mkono wako ikiwa hiyo ni kweli. Vema, kuwa na imani katika Mungu.

Unaona ninachomaanisha?

257 Vipi kuhusu baadhi yenu enyi watu ambao mnanijua? Una kitu moyoni mwako. Inua mkono wako. Wengi sana wenu! Siwezi kuifanya; lazima tu ije. Unajua, ni imani yako.

258 Georgie Bruce, namwona ameketi pale. Daima unajaribu kutafuta kitu kwa ajili ya mtu fulani, Georgie. Uliponywa, saratani. Hakuna swali akilini mwako. Siku uliyokuja kwenye maskani hii na kutoka nje kwa mlango huo, Roho Mtakatifu alikuja juu yangu, na kukuambia hapo hapo kitendo ambacho hakuna mtu ulimwenguni aliyejua isipokuwa wewe na Mungu na mtu mwingine. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hiyo ni kweli. Unaniamini, sivyo, Georgie? Una kitu moyoni

mwako, Georgie. Unaamini Mungu anaweza kuniambia kile kilichoko moyoni mwako?

Je, hiyo ingefanya ninyi wengine, watu wanaonijua, waamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

259 Namjua Georgie, lakini anafikiria jambo fulani. Ana watu wawili, ambao wako mbali na hapa, anaowaombea. Wote wawili wanaishi Corydon. Hiyo ni kweli. Naye ana mtu hapa, mwanamume anayemwombea, aliye nje hapa hospitalini. Na unaomba, sio sana kwa ajili ya uponyaji wake, lakini wokovu wa nafsi yake. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli, Georgie? Hiyo ni kweli kabisa.

260 Mtu fulani huko nyuma aliinua mkono wake, huko nyuma upande wa nyuma, nyuma hapa ndani. Wewe, vipi kukuhusu wewe? Waweza kuinua mkono wako, wewe ni mgeni kwangu? Mtu huyu anayeketi hapa akiniangalia, mimi sikujui. Je, unaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu, mtumishi wa Mungu? Unaamini Roho Mtakatifu, nilichosema ni Ukweli? Unaamini Hilo? [Ndugu huyo anasema, “Naam.”—Mh.] Ikiwa utaamini, umeto-. . .hicho ndicho kitu pekee ulicho nacho, maana unaugua saratani. Hiyo ni kweli. Wewe hutoki kwenye mji huu. Unatoka New Albany. Hiyo ni kweli. Na una saratani. Ikiwa utaamini kwa moyo wako wote, utapata afya. Je, utaikubali? Inua mkono wako. Atukuzwe Bwana.

261 Ninaamini, yule mwanamke huko nje na kofia inayoonekana nyeupe kwenye kichwa chake, mama mweusi, ameinua mkono wake. Bado sijapata mtu mweusi. Unaamini, mama? Naam, bwana, amini kwa moyo wako wote. Una shida ya moyo, shida ya tumbo, matatizo. Kuna mtu aliyekuleta hapa asubuhi ya leo. BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ni kweli, sivyo, mama? Ikiwa hiyo ni kweli, tikisa leso hiyo uliyo nayo mkononi mwako, ili watu waone. Sijawahi kumwona mwanamke huyo maishani mwangu.

262 Uliinua mkono wako? Je, mimi ni mgeni kwako? Na wewe mgeni kwangu. Unaamini Mungu ananijua, au Mungu anakujua? Unaamini anaweza kuniambia kilichoko moyoni mwako? Unamwombea mtu fulani. Ni baba yako, ana shida ya moyo. Hiyo ni kweli. Na unatafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu. BWANA ASEMA HIVI.

Ikiwa unaweza kuamini!

263 Vipi kuhusu maskini yule mama aliyeinua mkono wake *hivi,* unaamini? Shida yako ni upele huo mkononi mwako. Lakini unamwombea mjukuu. Hiyo ni kweli. Mtoto huyo si timamu. Hiyo ni kweli. Sivyo, mama? Amini kwa moyo wako wote, kwa ajili yake.

Wakati niliposema, “mtoto.” Ngoja kidogo. Loo, haya basi. Mwanao alipata ajali ya motokaa; kilema. Sikujui, mama, lakini hiyo ni kweli. Ikiwa hiyo ni kweli, inua mkono wako.

264 Sasa, ni Nani aliye hapa? Ni nani Huyo? Si mimi. Ninawezaje kufanya hivyo? Usiwe na ganzi kwa Roho, mambo ya Kiroho. Ni Mungu hapa! Roho Mtakatifu huyo unayemtaka, je, unamwamini sasa? Unamwamini sasa? Sawa, basi mpokee sasa. Sasa ndio wakati wa kumpokea. Amini kwa moyo wako wote.

265 Wewe uliye mgonjwa au mhitaji. Siwezi kuponya. Hakuna mtu anayeweza kuponya. Siwezi kutoa Roho Mtakatifu. Lakini yule anayeweza kuponya na kutoa Roho Mtakatifu, Yeye yupo hapa. Yeye Ndiye afanyaye hayo.

266 Sasa inamisheni vichwa vyenu. Aminini sasa hivi, ninapowaombeeni pamoja na leso hizi.

267 Baba yetu wa Mbinguni, kadiri nijuavyo, nilipitia kila mmoja ambao walikuwa ni wageni, kadiri nilivyojihisi kudhoofika na kuachilia; nilijisikia kuongozwa kwamba huu ndio wakati labda ambao Wateule wameona. Naomba kila mmoja wao, Bwana, aliyeitwa na kuruhusiwa kuitwa na Roho Wako; kitu fulani, imani yao, walikuwa na imani zaidi (baadhi yao) kuliko vile walivyofikiria walikuwa nayo. Wanaanza tu mioyoni mwao.

268 Na yule mwanamke aligusa vazi Lake wakati mmoja alipopita, Naye akageuka akasema, “Ni nani aliyenigusa?”

Wakasema, “Vema, kila mtu amekugusa.”

269 Akasema, “Lakini naona nimekuwa dhaifu.” Naye akampata maskini yule mwanamke akamwambia alikuwa anatokwa damu, na imani yake ilikuwa imemponya.

270 Na Biblia ilisema, kwamba, “Yeye angali ni Kuhani Mkuu, leo, awezaye kuguswa na hisia ya udhaifu wetu.” Maandiko yalisema, “Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.” Na ikiwa Yeye ni yule yule, na Kuhani Mkuu yule yule, atatenda vile vile na kufanya vile vile.

271 Na hebu watu waone kwamba Kanisa lililojazwa na Roho linakuja kwenye kichwa. Kristo anajiandaa kuja kuchukua Kanisa Lake. Ishara zake kubwa za mwisho, kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma; Yule aliyezungumza, akamjua Sara, na alijua alikuwa na mke aliyeitwa Sara, alimjua akiwa hemani alicheka; Yeye alisema, “Hiyo itakuwa ishara. Utakapoiona hiyo, kumbuka, kizazi hicho hakitapita mpaka yote yatimie.” Hii hapa. Tuko mwisho.

272 Jalia, Bwana, kwamba kila mtu mgonjwa hapa ajue kwamba Yesu Kristo aliye hai yuko hapa. Jalia leso hizi zibarikiwe kwa kila mwili mgonjwa ambao zinaendea. Ninamkemea ibilisi, kwa ajili ya watu. Ninamtorosha, kwa Roho wa Mungu, kwa imani, ninaondoa kila kivuli cha shaka. Naomba kila mtu hapa, aliyekusudiwa Uzima wa Milele, aipokee saa hii. Naomba kila ushirikina, kila kitulizo kidogo, kila kitu kidogo cha ulimwengu, kila mzigo mdogo, kama vile Biblia ilisema,

"Na tuweke kando kila mzigo, na dhambi ituzingayo kwa urahisi; ili tuweze kukimbia, kwa uvumilivu, mbio iliyowekwa mbele yetu; tukitazama" (kitu gani? kanisa? shirika?) "Mbuni na Mkamilishaji wa imani yetu," ambaye yuko hapa sasa, "Yesu Kristo, Mwana wa Mungu." Tukimtazama Yeye Yule... Haitulazimu kuchukua maneno ambayo tunajua kwamba ni kweli, lakini hata hivyo hayo Maneno yamefanywa halisi kwetu leo asubuhi. Yesu yule yule aliyekufa, hajafa, amefufuka tena, na miaka elfu mbili baadaye Yeye analeta Kanisa Lake kwenye kichwa. Roho ya Yuda inafanya kazi miongoni mwao. Lakini naomba waweke kando kila kikwazo na kila kitu, saa hii, na kumpokea Yeye.

273 Jalia wasikie, ambayo wamesikia, kupitia mahubiri. Naomba watambue sasa kwamba Maneno yale hasa waliyoyasikia yamedhihirika, nao wanayatambua, kwamba ni Kristo. Na sasa waweze kutenda, kuyafanyia kazi: kuyapokea, na kuinuka kwa miguu yao, watoe ushuhuda; na waingie katika Ufalme wa Mungu, kwa kujazwa na Roho Mtakatifu.

274 Wagonjwa na wapone. Wanaoteseka na waponywe. Jalia kila shauku ya moyo iwe sawa. Ijalie, Mungu Mwenyezi.

275 Sasa huku vichwa vyenu vimeinamishwa, mioyo yenu ikiwa wazi, jipe tu muda wa maombi; kabla tu, nadhani, ibada ya ubatizo inakuja, kabla tu ya hii. Kutakuwa na ibada nyingine usiku wa leo.

276 Sasa, kumbuka, usiache fursa hii ipite. Nimekuwa hapa sasa kwa saa mbili na nusu, au zaidi, nikijaribu kuchukua tu muda wangu, na kuleta Injili, na kuiweka ndani kikamilifu kabisa. Kisha tunakuja hadi mwisho. Na somo lenyewe: sikia, tambua, tenda. Usiache ipite juu ya kichwa chako. Umeisikia. Je, unatambua kwamba Uwepo Wake upo hapa? Je, unajua ni Yeye anayekuita? Basi iweke katika matendo. Mungu awe nawe. Kuwa na msimu wa maombi.

277 Ndugu Neville, njoo, kidogo, katika maombi, kama utakuja hapa.

Mshikilie tu juu.

*KUSIKIA, KUTAMBUA, KUTENDA KWA NENO LA MUNGU* SWA60-0221
(Hearing, Recognizing, Acting On The Word Of God)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 21 Februari, 1960, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org